Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Tisa

# Wakati wa Kanisa la Laodikia

Ufunuo 3:14-22

*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika;*

*Haya ndiyo anenayo Yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, Mwanzo wa Kuumba kwa Mungu.*

*Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto.*

*Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu.*

*Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.*

*Nakupa shauri ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*

*Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.*

*Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.*

*Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

**MJI WA LAODIKIA**

Jina hilo, Laodikia, ambalo maana yake ni, "haki za watu" lilitumiwa sana na lilipewa miji kadha kwa kuwaheshimu mabibi wa kifalme walioitwa hivyo. Mji huu ulikuwa mmoja wa miji iliyokuwa muhimu sana kisiasa na iliyostawi kibiashara sana katika Asia Ndogo. Mji huo ulipewa mali nyingi sana na wenyeji mashuhuri. Ulikuwa ni kituo cha shule kuu ya uuguzi. Watu wake walijulikana katika sanaa na sayansi. Mara nyingi uliitwa „mji mkuu wa nchi" kwa kuwa ulikuwa makao makuu ya nchi kwa miji mingine ishirini na mitano. Mungu wa kipagani aliyeabudiwa hapo alikuwa ni Zeu. Kwa kweli mji huu wakati mmoja uliitwa Diopolisi (Mji wa Zeu) kwa heshima ya mungu wao. Katika karne ya nne mkutano muhimu wa baraza la kanisa ulifanyika hapo. Matetemeko ya mara kwa mara ya ardhi hatimaye yalisababisha uhamwe kabisa.

Ni barabara jinsi gani sifa za wakati huu wa mwisho zilivyolingana kuuwakilisha wakati tunaoishi sasa. Kwa mfano, wao waliabudu mungu mmoja, Zeu, ambaye alikuwa ndiye mkuu na baba wa miungu. Hii ilitabiria kanuni ya kidini ya karne ya ishirini ya „Mungu mmoja, baba-yetu-sote" ambayo inaendeleza udugu wa binadamu, na hata sasa inawaunganisha Waprotestanti, Wakatoliki, Wayahudi, Wahindu, nk. kwa nia kwamba utaratibu wa ibada ya pamoja utaongezea upendo wetu na uelewano, na kutunzana. Wakatoliki na Waprotestanti hata sasa hivi wanajitahidi, na kwa kweli sasa hivi wanafaulu katika muungano huu wakiwa na nia dhahiri ya kwamba wengine wote watafuata. Nia hii hii ilionekana katika Umoja wa Mataifa wakati viongozi wa dunia walipokataa kutambua wazo lo lote moja la ibada ya kiroho lakini wakapendekeza kuwekea kando mawazo hayo yote mbalimbali wakiwa na matumaini ya kwamba dini zote zisawazishwe ziwe moja, kwa maana zote zina shauku ya madhumuni yale yale, zote zina makusudi yale yale, na zote kimsingi ni sahihi.

Angalia hilo jina, Laodikia, „haki za watu", ama „usawa wa watu." Je! kuliwahi kuwa na wakati kama wakati wa kanisa la karne ya ishirini ambao umeona mataifa YOTE yakiinuka na kudai usawa, wa watu na wa kiuchumi? Hizi ni siku za wakomunisti ambapo watu wote wanatakiwa kuwa sawa, ingawa inakuwa hivyo katika nadharia tu. Huu ni wakati wa vyama vya kisiasa vinavyojiita Wanademokrasia wa Kikristo, na Wajamaa wa Kikristo, Jumuiya ya Muungano wa Kikristo, nk. Kulingana na wanatheolojia wetu wenye mawazo huru Yesu alikuwa mwanaujamaa na kanisa la mwanzoni chini ya uongozi wa Roho liliendeleza ujamaa, na ati kwa hiyo inatupasa kufanya jambo hilo leo.

Watu wa zamani zile walipouita Laodikia kuwa mji mkuu wa nchi ilikuwa ni kutazamia serikali moja ya ulimwengu ambayo sasa tunaianzisha. Tunapowazia mji huo kuwa ndipo mahali pa baraza kuu la kanisa

tunaona zile jitihada za shughuli za ekumeni zinazofanyika siku hizi zikitangulia kuonyeshwa katika kivuli, ambapo hivi karibuni tutaona wote wale „wanaojiita" Wakristo wakiunganika pamoja. Kweli, kanisa na serikali, dini na siasa vinaungana. Magugu yanafungwa. Ngano hivi karibuni itakuwa tayari kwa kuwekwa ghalani.

Ulikuwa mji uliokumbwa na matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara, matetemeko ambayo hatimaye yaliuangamiza. Wakati huu utaishia na Mungu kuutikisa ulimwengu mzima ambao umeenda kufanya mapenzi na yule kahaba wa kale. Si kwamba tu taratibu za ulimwengu zitavunjika, bali dunia yenyewe itatikiswa kisha ifanywe upya kwa ajili ya ule utawala wa Kristo wa miaka elfu.

Huo mji ulikuwa tajiri, ulijaa mali nyingi. Ulikuwa umejaa utamaduni. Sayansi ilijaa. Jinsi ilivyo kama siku hizi. Makanisa ni matajiri. Ibada ni maridadi na zenye utaratibu, lakini ni baridi na zimekufa. Utamaduni na elimu vimechukua mahali pa Neno lililotolewa na Roho, na sayansi imepachukua mahali pa imani, hivi kwamba mwanadamu amechukuliwa mateka na mambo ya dunia.

Katika kila sifa Laodikia ya kale inaonekana imezaliwa katika Wakati wa Laodikia ya karne ya ishirini. Katika rehema za Mungu, naomba wale walio na sikio la kusikia watoke kwake wasije wakashiriki dhambi zake na hukumu inayofuata.

## WAKATI WA LAODIKIA

Wakati wa Laodikia ulianzia kwenye mwanzo wa Karne ya Ishirini, labda 1906. Utadumu muda gani? Utadumu muda gani? Mimi kama mtumishi wa Mungu ambaye amepata maono mengi sana, ambayo hakuna HATA MOJA limepata kukosa kutukia, hebu nibashiri (sikusema ninatabiri, lakini nabashiri) ya kwamba wakati huu utaishia kwenye mwaka wa 1977 hivi. Kama mtaruhusu maelezo mafupi hapa ya kibinafsi, ninawekea msingi ubashiri huu juu ya maono saba muhimu ya mfululizo ambayo yalinijia Jumapili moja asubuhi mwezi wa Juni, 1933. Bwana Yesu alinena nami na kusema ya kwamba kuja kwa Bwana kulikuwa kunakaribia, lakini ni kwamba kabla Yeye hajaja, matukio saba muhimu yangetukia. Niliyaandika yote asubuhi hiyo na kuutangaza ufunuo wa Bwana. Ono la kwanza lilikuwa kwamba Musolini angevamia Ethiopia na hilo taifa "litaanguka miguuni pake." Hilo ono hakika lilisababisha makelele miongoni mwa watu, na baadhi yao walikasirika sana niliposema jambo hilo nao hawangeliamini. Lakini ilitendeka namna hiyo. Yeye aliingia tu humo akiwa na silaha zake za kisasa na kuitwaa. Wananchi hawakuweza kufanya kitu cho chote. Lakini lile ono pia lilisema ya kwamba Musolini angefikia mwisho mbaya sana hapo watu wake mwenyewe watakapomgeuka wamshambulie. Hilo lilikuja kutimia sawa kabisa na ilivyosemwa.

Ono lililofuatia lilitabiri ya kwamba Mwaaustria jina lake Adolf Hitler atainuka kama mtawala wa mabavu huko Ujerumani, na ya kwamba angeuingiza ulimwengu katika vita. Lilionyesha boma la Siegfried na jinsi ambavyo majeshi yetu yangekuwa na wakati mgumu sana kuliteka. Kisha likaonyesha ya kwamba Hitler atafikia mwisho usiojulikana.

Ono la tatu lilihusu mazingira ya siasa za ulimwengu kwa kuwa lilinionyesha ya kwamba kutakuweko na ITIKADI tatu kuu, Ufashisti, Unazi, Ukomunisti, lakini ni kwamba zile mbili za kwanza zingemezwa katika ile ya tatu. Hiyo sauti ikaonya, ANGALIA URUSI, ANGALIA URUSI. Mtazme sana Mfalme wa Kaskazini."

Ono la nne lilionyesha maendeleo makubwa katika sayansi ambayo yangekuja baada ya vita vya pili vya ulimwengu. Yalifikia kilele katika ono la gari la plastiki mfano wa futuza kwa juu nayo ilikuwa ikikimbia kwenye barabara kuu nzuri ikiongozwa na rimoti hivi kwamba watu walionekane wameketi ndani ya gari hili lisilo na usukani nao walikuwa wakicheza namna fulani ya mchezo wa kujifurahisha.

Ono la tano lilihusu shida ya uadilifu wa wakati wetu, ikihusu zaidi sana wanawake. Mungu alinionyesha ya kwamba wanawake walianza kutoka kwenye nafasi yao waliporuhusiwa kupiga kura. Ndipo wakakata nywele zao, jambo ambalo lilionesha ya kwamba hawakuwa tena chini ya mamlaka ya mwanamume lakini walisisitiza wapewe haki sawa, ama mara nyingi sana, zaidi ya haki sawa. Akaingilia kuvaa nguo za kiume na kuendea hali ya kwenda uchi, mpaka picha ya mwisho niliyoona ilikuwa ni ya mwanamke aliyekuwa uchi akiwa tu na kijiaproni kidogo kama cha jani la mtini. Kwa ono hili niliona upotovu mbaya sana na hali mbaya ya uadilifu wa ulimwengu mzima.

Ndipo katika ono la sita aliinuka huko Marekani mwanamke mrembo sana, lakini katili. Yeye alishikilia watu kwa nguvu zake zote. Niliamini ya kwamba hii ilikuwa ni kuinuka kwa Kanisa Katoliki la Kirumi, ingawa nilijua huenda ikawa ni ono la mwanamke fulani akiinuka katika mamlaka kuu huko Marekani kwa kura ya kupendwa na wanawake.

Ono la mwisho na la saba lilikuwa ambapo nilisikia mlipuko wa kutisha sana. Nilipogeuka kuangalia sikuona kitu ila mabaki ya nyumba, mashimo kama ya volkeno, na moshi kila mahali juu ya nchi ya Marekani.

Kwa msingi wa maono haya saba, pamoja na mabadiliko ya haraka ambayo yameenea ulimwenguni katika miaka hamsini iliyopita, NINABASHIRI (mimi si tabiri) ya kwamba maono haya yote yatakuwa

yametimia ifikapo mwaka wa 1977. Na ingawa wengi wanaweza kuona ya kwamba tamshi hili si la kuaminiwa kwa sababu ya ukweli kwamba Yesu alisema ya kwamba „hakuna mtu aijuaye siku hiyo wala saa," Ningali ninashikilia ubashiri huu baada ya miaka thelathini kwa sababu, Yesu HAKUSEMA hakuna mtu angeweza kujua mwaka, mwezi ama juma ambapo kuja Kwake kutakamilishwa. Kwa hiyo ninarudia, ninaamini kwa kweli na kushikilia kama mwanafunzi binafsi wa Neno, pamoja nauongozi wa Kiungu ya kwamba mwaka wa 1977 unapaswa kumaliza taratibu za ulimwengu na kufungulia mlango ule utawala wa miaka elfu.

Sasa hebu niseme jambo hili. Kuna mtu ye yote anayeweza kuthibitisha lo lote la maono hayo kuwa yamekosea? Je! yote hayakutimizwa? Naam, kila moja limetimizwa, ama liko katika hatua za kutimizwa sasa hivi. Musolini aliivamia Ethiopia akashinda, kisha akaanguka na kuipoteza yote. Hitler alianza vita ambavyo hakuweza kuvimaliza na akafa namna isivyojulikana. Ukomunisti ulimeza ITIKADI hizo nyingine mbili. Ile motokaa ya plastiki mfano wa futuza imeundwa tayari na inangojea kuanzishwa kwa utaratibu mzuri zaidi wa barabara. Wanawake karibu wote wako uchi, na hata hivi sasa wanavaa vazi la kuogelea ambalo halifuniki kifua. Na hivi majuzi tu niliona kwenye gazeti nguo ile ile hasa niliyoona katika ono langu (kama unaweza kuiita nguo). Ilikuwa nguo ya namna ya plastiki inayoona ikiwa na visehemu vitatu vyeusi ambavyo vilifunika sehemu ndogo ya matiti, halafu kulikuwako na mahali peusi kama aproni ndogo sehemu ya chini. Kanisa Katoliki linaendelea kupamba moto. Tumekuwa na rais mmoja Mkatoliki na bila shaka tutakuwa na mwingine.

Ni kitu gani kilichosalia? Hakuna kitu ila Waebrania 12:26. *"Ambaye sauti Yake iliitetemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia."* Mara nyingine tena Mungu ataitetemesha nchi na pamoja nayo atatetemesha na kulegeza kila kitu kinachoweza kutetemeshwa. Ndipo Yeye ataifanya upya. Mwezi wa Marchi hivi karibuni tu, mwaka wa 1964, lile tetemeko la ardhi la Ijumaa Kuu la Alaska liliutikisa ulimwengu mzima ingawa halikuuondoa mahali pake. Lakini Mungu alikuwa akionya kwa tetemeko la ardhi la dunia nzima yale atakayofanya hivi karibuni kwa kiwango kikubwa zaidi. Yeye ataulipua na kuutetemesha ulimwengu huu uliolaaniwa kwa dhambi, ndugu yangu, dada yangu, na kuna mahali pamoja tu panapoweza kustahimili msukosuko huo, na hapo ni katika zizi la Bwana Yesu. Na ningewasihi wakati rehema ya Mungu ingali inapatikana kwa ajili yako, kwamba uyatoe maisha yako yote, kabisa kikamilifu kwa Yesu Kristo, Ambaye kama Mchungaji wa kweli atakuokoa na kukulinda na kukuweka katika utukufu bila mawaa kwa furaha kuu.

**MJUMBE**

Natilia shaka sana kama wakati wo wote ule kweli ulimjua mjumbe ambaye Mungu alimtuma kwa wakati huo, isipokuwa katika wakati wa kwanza ambapo Paulo alikuwa ndiye mjumbe. Na hata katika wakati huo wengi hawakumtambua kwa kile alichokuwa.

Sasa wakati tunaoishi utakuwa mfupi sana. Matukio yatatukia haraka sana. Kwa hiyo mjumbe wa Wakati huu wa Laodikia hana budi kuwa yupo hapa hivi sasa, ingawa labda bado hatumjui. Lakini hapana budi patakuwa na wakati ambapo atapata kujulikana. Sasa naweza kuwathibitishia jambo hilo kwa sababu tuna Andiko linaloeleza huduma yake.

Kwanza kabisa, mjumbe huyo atakuwa nabii. Yeye atakuwa na utume wa nabii. Yeye atakuwa na huduma ya kinabii. Itakuwa na msingi imara kabisa juu ya Neno kwa sababu wakati atakapotoa unabii ama kuona ono, daima litakuwa "linaloelekea kwenye Neno" na DAIMA litatimia. Yeye atathibitishwa kama nabii kwa sababu ya usahihi wake.

Ushahidi wa kwamba yeye ni nabii unapatikana katika Ufunuo 10:7

> *"Isipokuwa katika siku za sauti ya mjumbe wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi Wake hao manabii."*

Sasa mtu huyu, ambaye katika aya hii anaitwa „malaika" katika toleo la King James SI kiumbe cha mbinguni. Yule malaika wa sita anayepiga baragumu, ambaye ni kiumbe cha mbinguni, yuko katika Ufu. 9:13, na wa saba wa mpango huo huo yuko katika Ufu. 11:15. Huyu hapa katika Ufu. 10:7 ni mjumbe wa wakati wa saba na ni mwanadamu, naye anapaswa kuleta ujumbe kutoka kwa Mungu, na ujumbe wake na huduma yake itamaliza siri ya Mungu kama alivyowahubiri watumishi Wake, manabii. Mungu atamchukua mjumbe huyu wa mwisho kama nabii KWA SABABU YEYE NI NABII. Hivyo ndivyo Paulo alivyokuwa katika wakati wa kwanza, na wakati wa mwisho unaye mmoja, pia.

Amosi 3:6-7,

> *"Je! tarumbeta itapigwa mjini, watu wasiogope? Mji utapatikana na hali mbaya, asiyoileta Bwana?*
>
> *Hakika Bwana Mungu hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi Wake manabii siri Yake."*

Ni katika wakati wa mwisho ambapo ndipo zile ngurumo saba za Yesu zilipotoa sauti zao. Ufunuo 10:3-4,

> *"Naye akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo. Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao.*
>
> *Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike."*

Kile kilichokuwa kwenye ngurumo hizo hakuna ajuaye. Lakini tunahitaji kujua. Na itatakiwa nabii kupata ufunuo kwa maana Mungu hana njia nyingine ya kutoa mafunuo Yake ya Kimaandiko ila kwa njia ya nabii. Neno daima lilimjia nabii na daima litamjia. Kwamba hii ni sheria ya Mungu ni dhahiri kwa hata kuchunguza kwa purukushani Maandiko. Mungu asiyebadilika akiwa na njia zisizobadilika alimtuma nabii Wake katika kila wakati ambapo watu walikuwa wameondoka kutoka kwenye utaratibu wa Mungu. Wanaatheolojia pamoja na watu wakiwa wameondoka kwenye Neno, Mungu daima alimtuma mtumishi Wake kwa watu hawa (lakini mbali na wanatheolojia) ili asahihishe mafundisho ya uongo na kuwaongoza watu wamrudie Mungu.

Kwa hiyo tunaona mjumbe wa wakati wa saba akija, naye ni nabii.

Si kwamba tu tunamwona mjumbe huyu akija hapa katika Ufu. 10:7, lakini tunaona ya kwamba Neno linazungumza juu ya Eliya akija kabla ya Yesu kurudi.

Katika Mathayo 17:10,

> *"Wanafunzi Wake wakamwuliza, wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?" Yesu akajibu, "Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote."*
>
> *Kabla ya kule kuja kwa Bwana wetu, Eliya hana budi kurudi kwa ajili ya kazi ya kurudisha yaliyopotezwa katika kanisa.*

Hivi ndivyo Malaki 4:5 inavyosema,

> *"Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana."*

Hakuna shaka kabisa kwamba Eliya hana budi kurudi kabla ya kuja kwa Yesu. Yeye ana kazi maalum ya kutimiza. Kazi hiyo ni sehemu ile ya Mal. 4-6 inayosema "ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." Sababu ya kwamba sisi tunajua hii ndiyo kazi yake maalum ya kufanya katika wakati huo ni kwa sababu tayari ametimiza sehemu ile inayosema "ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao," wakati huduma ya Eliya ilipokuwa hapa katika Yohana Mbatizaji.

Luka 1:17,

> *"Naye atatangulia mbele Zake katika Roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa."*

Katika huduma ya Yohana "mioyo ya baba iligeuzwa ikawaelekea watoto wao." Tunajua hilo kwa sababu Yesu alisema hivyo. Lakini haisemi ya kwamba mioyo ya watoto ilielekezwa kwa baba zao. Hilo bado halijatukia. Mioyo ya watoto wa siku za mwisho itageuzwa iwaelekee mababa wa Kipentekoste. Yohana aliwatayarisha mababa kwa ajili ya Yesu kuwakaribisha watoto waingie zizini. Sasa nabii huyu ambaye atashukiwa na Roho ya Eliya atawatayarisha watoto wapate kumkaribisha Yesu.

Yesu alimwita Yohana Mbatizaji, Eliya.

Mathayo 17:12,

> *"Ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka."*

*Sababu ya kumwita Yohana Eliya, ilikuwa ni kwa sababu Roho yule yule aliyekuwa kwa Eliya alikuwa amekuja juu ya Yohana, kama vile Roho huyo alivyokuwa amemrudia Elisha baada ya utawala wa Mfalme Ahabu.* Sasa mara nyingine tena Roho huyo atarudi juu ya mtu mwingine kabla tu ya Yesu kuja. Yeye atakuwa nabii. Yeye atathibitishwa hivyo na Mungu. Kwa kuwa Yesu, Mwenyewe, katika mwili hatakuwa hapa kumthibitisha, (kama alivyomfanyia Yohana) jambo hilo litafanywa na Roho Mtakatifu hivi kwamba huduma ya nabii huyu itafuatwa na madhihirisho makuu na ya ajabu. Kama nabii, kila ufunuo utadhihirishwa, kwa maana kila ufunuo utatimia. Matendo ya ajabu ya nguvu yatatendwa kwa amri zake

katika imani. Ndipo utaletwa ujumbe ambao Mungu amempa yeye katika Neno kuwarudisha watu kwenye kweli na nguvu za kweli za Mungu. Wengine watasikiliza, lakini walio wengi watafanya kama ilivyo kawaida na kumkataa yeye.

Kwa kuwa huyu nabii mjumbe wa Ufu. 10:7 atakuwa ni yule yule wa Mal. 4:5-6 yeye atakuwa bila shaka kama Eliya na Yohana. Wote wawili walikuwa watu waliotengwa kutoka kwenye shule za dini zilizokubalika za siku zao. Wote wawili walikuwa watu wa nyikani. Wote wawili walitenda kazi tu wakati walipokuwa na "Bwana asema hivi," moja kwa moja kutoka kwa Mungu kwa ufunuo. Wote wawili walikemea taratibu za dini na viongozi wa siku zao. Lakini si hivyo tu, wao waliwakemea wote waliokuwa wamepotoka ama wanawapotosha wengine. Na tazama, wote wawili walitabiri sana dhidi ya wanawake wazinzi na njia zao. Eliya alimkemea Yezebeli, na Yohana akamkemea Herodia, mke wa Filipo.

Ingawa hatapendwa sana na watu, yeye atathibitishwa na Mungu. Kama vile Yesu alivyomthibitisha Yohana, na Roho Mtakatifu akamthibitisha Yesu, tunaweza kabisa kutarajia mtu huyu kwanza atathibitishwa na Roho akitenda kazi katika maisha yake katika matendo ya nguvu ambayo hayawezi kukanushwa na yasiyoonekana mahali pengine po pote; naye Yesu Mwenyewe, katika kurudi, atamthibitisha, kama vile alivyomthibitisha Yohana. Yohana alishuhudia ya kwamba Yesu anakuja,_vivyo hivyo na mtu huyu pia, kama Yohana, atashuhudia ya kwamba Yesu anakuja. Na kule kurudi kwenyewe kwa Kristo kutathibitisha ya kwamba mtu huyu kweli alikuwa mtangulizi wa kuja Kwake kwa mara ya pili. Huu ndio uthibitisho wa mwisho ya kwamba huyu kweli ndiye nabii wa Mal. 4, kwa maana mwisho wa wakati wa Mataita utakuwa ni Yesu, Mwenyewe, akitokea. Ndipo wale ambao wamemkataa watakuwa wamechelewa wale ambao wamemkataa.

Kusudi tuelezee zaidi maelezo yetu ya nabii huyu wa siku za mwisho, hebu na tuone waziwazi kwamba yule nabii wa Mat. 11:12, alikuwa ni Yohana Mbatizaji, ambaye ndiye aliyetabiriwa katika Mal. 3:1,

> *"Angalieni, namtuma mjumbe Wangu, Naye ataitengeneza njia mbele Yangu; Naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu Lake ghafula, naam, yule Mjumbe wa Agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa Majeshi."*

Mathayo 11:1-12,

> *"Ikawa Yesu alipokwisha kuwaagiza wanafunzi Wake kumi na wawili, alitoka huko kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao.*
>
> *Naye Yohana aliposikia huko gerezani matendo Yake Kristo, alituma wanafunzi wake wawili,*
>
> *kumwuliza, Wewe Ndiwe Yule ajaye, au tumtazamie mwingine?*
>
> *Yesu akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana tena mnayoyasikia na kuyaona;*
>
> *vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa Habari Njema.*
>
> *Naye heri awaye yote asiyechukizwa Nami.*
>
> *Na hao walipokwenda zao, Yesu alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, Mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo?*
>
> *Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? Tazama, watu wavaao mavazi mororo wamo katika nyumba za wafalme.*
>
> *Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Ni kuona nabii? naam, nawaambia, na aliye mkuu zaidi ya nabii.*
>
> *Kwa maana huyu ndiye aliyeandikiwa haya, Tazama, Mimi namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia Yako mbele Yako.*
>
> *Amin, nawaambieni, hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji; walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye."*

Hili tayari limetukia. Hili limetukia. Limekwisha. Lakini angalia sasa katika Malaki 4:1-6,

> *"Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi.*
>
> *Lakini kwenu ninyi mnaolicha Jina Langu, Jua la Haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa Zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza- cheza kama ndama wa mazizini.*

*Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi.*

*Ikumbukeni torati ya Musa, mtumishi Wangu, niliyomwamuru huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, naam, amri na hukumu.*

*Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya.*

*Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana.*"

*Mnaona, mara baada ya kuja kwa Eliya HUYU, dunia itatakaswa kwa moto na watendao uovu watateketezwa wawe majivu.* Bila shaka, hili HALIKUTENDEKA wakati wa Yohana (yule Eliya wa siku hizo.) Roho wa Mungu aliyetabiri kuja kwa yule mjumbe katika Mal. 3:1 (Yohana) alikuwa tu akirudia lile tamshi Lake la hapo awali la kinabii la Isa. 40:3 lililotamkwa karne zisizopungua tatu hapo kabla.

*"Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana; nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu."*

Sasa Yohana, kwa Roho Mtakatifu, ni sauti iliyonenwa na Isaya na Malaki katika Mat. 3:3,

*"Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito Yake."*

Kwa hiyo tunaweza kuona vizuri kutoka kwenye Maandiko haya ya kwamba yule nabii katika Mal. 3, ambaye alikuwa ni Yohana, HAKUWA yule nabii wa Mal. 4, ingawa kweli, Yohana na nabii huyu wa siku za mwisho pia wana Roho yule yule aliyekuwa juu ya Eliya.

Sasa mjumbe huyu wa Mal. 4 na Ufu. 10:7 atafanya mambo mawili. Moja: Kulingana na Mal. 4 ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao. Pili: Atafunua siri za ngurumo saba katika Ufu. 10 ambazo ni mafunuo yale yaliyo ndani ya zile muhuri saba. Hizi „kweli za kisiri" zilizofunuliwa Kiungu ndizo zitakazoigeuza kweli mioyo ya watoto iwaelekee baba zao wa Kipentekoste. Ndio hivyo kabisa.

Lakini fikiria hili pia. Huyu nabii-mjumbe atakuwa katika hali yake na tabia zake kama walivyokuwa Eliya na Yohana. Watu wa siku za huyu nabii-mjumbe watakuwa kama walivyokuwa katika siku za Ahabu, na katika za Yohana. Na kwa kuwa ni "WATOTO PEKE YAO" ambao mioyo yao itageuzwa, watoto tu ndio watakaosikiliza. Katika siku za Ahabu kulipatikana mzao wa kweli wa Waisraeli 7,000 tu. Katika siku za Yohana kulikuwa pia na wachache sana. Umati mkubwa katika nyakati hizo zote mbili ulikuwa katika uasherati wa ibada za sanamu.

Nataka kulinganisha mara moja tena kati ya nabii-mjumbe wa Laodikia na Yohana, nabii-mjumbe ambaye alikutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo. Watu katika siku za Yohana walikosea wakimdhania kuwa ndiye Masihi.

Yohana 1:19-20,

*"Na huu ndio ushuhuda wake Yohana, Wayahudi walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalemu ili wamwulize, Wewe u nani? Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba, Mimi siye Kristo."*

Sasa huyu nabii-mjumbe wa siku za mwisho atakuwa na nguvu sana mbele za Bwana hivi kwamba kutakuweko na wale watakaomdhania kwamba yeye ni Bwana Yesu.

(Kutakuwako na roho fulani katika siku za mwisho ambayo itawashawishi baadhi ya watu na kuwafanya waamini jambo hili.

Mathayo 24:23- 26,

*"Kwa maana watatokea Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.*

*Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.*

*Basi wakiwaambia, Tazama, Yuko jangwani, msitoke; tazama, Yumo nyumbani, msisadiki.")*

Lakini msiamini jambo hilo. Yeye si Yesu Kristo. Yeye si Mwana wa Mungu. YEYE NI MMOJA WA NDUGU, NABII, MJUMBE, MTUMISHI WA MUNGU. Hahitaji kupewa heshima kubwa zaidi kuliko ile Yohana aliyopokea wakati alipokuwa sauti iliyolia, "Mimi Siye, LAKINI ANAKUJA BAADA YANGU."

Kabla hatujafunga sehemu hii juu ya mjumbe wa Wakati wa Laodikia, hatuna budi kuyachunguza mawazo haya mawili kwa makini sana. Kwanza, wakati huu utakuwa na Nabii-Mjumbe mmoja. Ufu. 10:7,

inasema, "Atakapokuwa yeye (umoja) tayari kupiga baragumu." Hapajatokea wakati ambapo Mungu aliwapa watu Wake manabii wawili wakuu kwa wakati mmoja. Yeye alimtoa Henoko (peke yake); alimtoa Nuhu (peke yake); alimtoa Musa (yeye pekee ndiye aliyekuwa na Neno ingawa wengine walitabiri); Yonana Mbatizaji alikuja PEKE YAKE. Sasa katika siku hii ya mwisho kutakuwako na NABII (si nabii mke_ingawa katika wakati huu kuna wanawake wengi kuliko wanaume wanaodai kutoa ufunuo wa Mungu), na Neno lisiloweza kukosea linasema ya kwamba yeye (nabii huyo) atawafunulia watu wa wakati wa mwisho siri, na kuigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.

Kuna wale wanaosema ya kwamba watu wa Mungu watakusanyika pamoja kwa ufunuo wa pamoja. Ninapinga tamshi hilo. Ni wazo tu, lisilohakikishwa mbele ya Ufu. 10:7. Sasa mimi sikatai ya kwamba watu watatabiri katika wakati huu wa mwisho na huduma zao zinaweza na zitakuwa sahihi. Sikatai ya kwamba kutakuwako na manabii kama vile katika siku za Paulo ambapo kulikuwa na "nabii mmoja jina lake Agabo aliyetabiri juu ya njaa kubwa." Ninakubali ya kwamba ndivyo ilivyo. LAKINI NINAKATAA JUU YA USHUHUDA USIOKOSEA WA NENO YA KWAMBA KUNA NABII-MJUMBE ZAIDI YA MMOJA AMBAYE ATAFUNUA SIRI ZILIZO KATIKA NENO, NA AMBAYE ANA HUDUMA YA KUIGEUZA MIOYO YA WATOTO IWAELEKEE BABA ZAO. "Bwana asema hivi" kwa Neno Lake lisilokosea inasimama, na litasimama na kuthibitishwa. Kuna nabii-mjumbe mmoja kwa wakati huu.

Juu ya msingi wa tabia za wanadamu peke yake, mtu ye yote anajua ya kwamba palipo na watu wengi kuna hata na maoni yasiyopatana juu ya mambo madogo-madogo ya fundisho muhimu ambalo wote wanashikilia pamoja. Ni nani basi atakayekuwa na mamlaka ya kutokosea ambayo itarudishwa katika wakati huu wa mwisho, kwa kuwa wakati huu wa mwisho utarudi kwenye kumdhihirisha Bibi-arusi wa Neno Halisi? Hiyo inamaanisha tutakuwa na Neno tena kama lilivyotolewa kikamilifu, na kueleweka kikamilifu katika siku za Paulo. Nitakwambia ni nani atakayekuwa nalo. Itakuwa ni nabii aliyethibitishwa kinaganaga, ama hata aliyethibitishwa kinaganaga zaidi kuliko nabii ye yote katika nyakati zote tangu Henoko hata siku hii, kwa sababu mtu huyu itambidi kuwa na huduma ya jiwe la kifuniko, na Mungu atamtambulisha. Haitambidi kujitetea, Mungu atamtetea kwa sauti ya ishara. Amina.

Wazo la pili linalopaswa kutiwa mioyoni mwetu ni ya kwamba zile nyakati saba za kanisa zilianzia na roho wa mpinga-Kristo pamoja na Roho Mtakatifu Ambaye ni wa kubarikiwa milele.

I Yohana 4:1,

> *"Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani."*

Mliona jambo hilo? Roho wa mpinga-Kristo anatambulishwa na manabii wa uongo. Nyakati hizi zilikuja pamoja na manabii wa uongo na zitaisha na manabii wa uongo. Sasa bila shaka kutakuwako na NABII HALISI WA UONGO katika maana ya kujitokeza kabisa kwa mtu huyo aliyetajwa katika Ufunuo. Lakini kwa sasa kabla ya kufunuliwa kwake kutatokea manabii wengi wa uongo.

Mathayo 24:23- 26,

> *"Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule, msisadiki.*
>
> *Kwa maana watatokea Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.*
>
> *Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele.*
>
> *Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; tazama, Yumo nyumbani, msisadiki."*

Manabii hawa wa uongo wametiwa alama kwa ajili yetu katika Maandiko mengine mbalimbali kama haya yafuatayo.

II Petro 2:1-2,

> *"Lakini kuliondokea manabii wa uongo pia katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia.*
>
> *Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa."*

II Timotheo 4:3-4,

> *"Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti;*
>
> *Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo."*

I Timotheo 4:1,

*"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani."*

Sasa katika kila hali utaona ya kwamba nabii wa uongo ni yule aliye nje ya Neno. Kama tu vile tulivyowaonyesha ya kwamba „mpinga-Kristo" maana yake ni „mpinga-Neno" hivyo basi hawa manabii wa uongo wanakuja wakilipotosha Neno, wakilipa maana fulani inayokubaliana na nia zao za kishetani. Je! umewahi kuona jinsi watu wanavyowapotosha wengine wanavyowafunga watu na kuwakaza kwao kwa hofu? Wao wanasema ya kwamba kama watu hawafanyi wanalosema wao, ama wakiondoka, basi maangamizi yatafuata. Wao ni manabii wa uongo, kwa kuwa nabii wa kweli daima atamwongoza mtu kwenye Neno na kuwafunga watu kwa Yesu Kristo naye hatawaambia watu wamwogope yeye ama yale anayosema, lakini waogope yale Neno lisemayo. Angalia jinsi watu hawa kama vile Yuda wanavyokimbilia fedha. Wanakufanya uuze mali yote uliyo nayo na uitoe kwao na kwenye miradi yao. Wanatumia wakati mwingi zaidi katika matoleo kuliko katika Neno. Wale wanaojaribu kutumia karama watatumia karama ambayo ina makosa kidogo ndani yake kisha waombe watu fedha, na wawekee kando Neno na kuita jambo hilo ni la Mungu. Nao watu watawaendea, na kuwavumilia, na kuwaunga mkono, na kuwaamini, bila kujua ni njia ya mauti.

Naam, nchi imejaa waigaji wa kimwili. Katika siku hiyo ya mwisho watajaribu kumwiga yule nabii-mjumbe. Wale wana saba wa Skewa walijaribu kumwiga Paulo. Simoni mchawi alijaribu kumwiga Petro. Uigaji wao utakuwa wa kimwili. Hawataweza kufanya kile nabii wa kweli anachofanya. Wakati atakaposema ufufuo umekwisha watazunguka-zunguka wakidai ufunuo mkuu ya kwamba kile watu walicho nacho ni kweli kabisa na ati Mungu atatenda mambo makubwa zaidi na ya ajabu zaidi miongoni mwa watu. Nao watu watadanganywa na hayo. Manabii wawa hawa wa uongo watadai ya kwamba mjumbe wa siku za mwisho si mwanatheolojia, kwa hiyo hapaswi kusikilizwa. Hawataweza kufanya kile huyo mjumbe anachoweza kufanya; hawatathibitishwa na Mungu kama nabii huyo wa siku za mwisho atakavyothibitishwa, lakini kwa maneno yao makubwa makubwa na kwa uzito wa umaarufu wao ulioenea ulimwengu mzima wao watawaonya watu wasimsikilize mtu huyo (mjumbe) nao watasema yeye anafundisha makosa. Wao wanafanya kabisa kama baba zao, wale Mafarisayo, waliokuwa wa ibilisi, kwa kuwa walidai ya kwamba pia Yohana na Yesu wote wawili walifundisha makosa.

Sasa kwa nini hawa manabii wa uongo wanampinga nabii wa kweli na kudharau mafundisho yake? Kwa sababu wanafanya vile vile walivyofanya baba zao katika siku za wakati wa Ahabu walimpinga Mikaya. Kulikuwa na jumla ya watu mia nne na wote walikubaliana; na wote wakisema jambo lile lile, waliwadanganya watu. Lakini nabii MMOJA—mmoja tu—alikuwa sahihi na hao wengine wote walikuwa makosani kwa sababu Mungu alikuwa ametoa ufunuo KWA MMOJA TU.

Jihadharini na manabii wa uongo, kwa maana wao ni mbwa mwitu wakali.

Kama ungali una mashaka yo yote juu ya jambo hili mwombe Mungu kwa Roho Wake akujaze na kukuongoza, KWA MAANA WALIO WATEULE HAWAWEZI KUPUMBAZWA. Ulilipata jambo hilo? Hakuna mtu ye yote anayeweza kukupumbaza. Paulo asingeweza kumdanganya mteule yeyote, kama angekuwa amekosea. Na katika wakati huo wa kwanza wa Efeso wateule kule wasingeweza kudanganywa kwa kuwa waliwajaribu mitume wa uongo na manabii na kuwaona kuwa ni waongo na kuwafukuza. Haleluya. Kondoo WAKE wanaisikia sauti Yake na kumfuata YEYE. Amina. Ninaamini jambo hilo.

**SALAMU**

Ufunuo 3:14,

*"Haya ndiyo anenayo Yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa Kweli, Mwanzo wa Kuumba kwa Mungu."*

Jamani, je! hayo siyo maelezo mazuri sana kuliko yote ya sifa za Bwana na Mwokozi wetu anayependeza sana, Yesu Kristo? Maneno haya karibu yananifanya nipige makelele. Yanaleta roho ya mambo halisi sana moyoni mwangu. Kuyasoma tu bila hata ya kungojea ufunuo wa kindani wa Roho juu yake kunanifurahisha sana.

Yesu anatupa sifa hii Yake kuhusiana na wakati wa mwisho. Siku za neema zinakwisha. Yeye ameangalia tokea karne ya kwanza moja kwa moja mpaka ya ishirini, na kutuambia mambo yote yanayohusu nyakati hizi. Kabla ya Yeye kutufunulia tabia za wakati wa mwisho, anatupa mtazamo mmoja wa mwisho wa Uungu Wake mkuu wa neema. Huu ni ufunuo wa jiwe la kifuniko wa nafsi Yake.

Haya ndiyo anenayo Yeye aliye "AMINA". Yesu ni Amina wa Mungu. Yesu ni "Na Iwe Hivyo" ya Mungu. Amina inawakilisha mwisho. Inawakilisha kibali. Inawakilisha ahadi ya ushindi. Inawakilisha ahadi isiyobadilika. Inawakilisha muhuri ya Mungu.

Ninataka mwangalie jambo hili kwa makini sasa uone jambo fulani tamu sana na la kupendeza. Nilisema huu ni ufunuo wa wakati wa mwisho wa nafsi Yake Mwenyewe. Wakati siku ya neema itakapokwisha, ndipo ule utawala wa miaka elfu unapokuja baada ya muda mfupi, sivyo?

Vema, soma pamoja nami Isaya 65:16-19.

*"Hata itakuwa yeye atakayejibariki duniani, atajibariki kwa Mungu wa kweli; naye atakayeapa duniani, ataapa kwa Mungu wa kweli; kwa kuwa taabu za kwanza zimesahauliwa, na kwa kuwa zimefichwa machoni Pangu.*

*Maana, tazama, Mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni.*

*Lakini furahini, mkashangilie daima, kwa ajili ya hivi niviumbavyo; maana, tazama, naumba Yerusalemu uwe shangwe, na watu wake wawe furaha.*

*Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawonea shangwe watu wangu; sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, wala sauti ya kuomboleza."*

Hii ni kuhusu Yerusalemu Mpya. Huu ndio ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini tunapoingia katika ule utawala wa miaka elfu, sikia analosema juu ya kuwa namna fulani ya Mungu, aya ya 16,

*"Hata itakuwa yeye atakayejibariki duniani atajibariki kwa Mungu wa kweli."*

*Naam, hiyo ni kweli, lakini tafsiri halisi si "Mungu wa kweli."* Ni "Mungu wa AMINA". Kwa hiyo tunasoma, "Atajibariki kwa Mungu wa AMINA; naye atakayeapa duniani, ataapa kwa Mungu wa AMINA; Kwa maana taabu za kwanza zimesahauliwa, na kwa kuwa zimefichwa machoni Pangu. Maana, tazama, Mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni. Lakini furahini, mkashangilie daima, kwa ajili ya hivi niviumbavyo; maana, tazama, naumba Yerusalemu uwe shangwe, na watu wake wawe furaha. Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawonea shangwe watu Wangu; na sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, wala sauti ya kuomboleza." Haleluya. Huyu hapa Yehova wa Agano la Kale, "Mungu wa Amina." Huyu hapa Yesu wa Agano Jipya, "Mungu wa Amina". Sikilizeni, Enyi Israeli, Bwana Mungu wako ni Mungu MMOJA. Hilo hapo tena, Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa Agano Jipya. "Sikilizeni, Enyi, Israeli Bwana Mungu wako ni Mungu MMOJA." Agano Jipya halimfunui Mungu MWINGINE, ni ufunuo zaidi wa MUNGU MMOJA NA YEYE YULE. Kristo hakuja kujitambulisha Mwenyewe. Yeye hakuja kumfunua Mwana. Alikuja kumfunua na kumfanya Baba ajulikane. Yeye hakunena kamwe juu ya Miungu miwili; alinena juu ya Mungu MMOJA. Na sasa katika wakati huu wa mwisho, tumerudi kwenye ufunuo wa jiwe la kifuniko, ufunuo mkubwa wa Uungu kuliko mafunuo yote katika Biblia nzima, yaani, YESU NI MUNGU, YEYE NA BABA NI MMOJA: KUNA MUNGU MMOJA, NA JINA LAKE NI BWANA YESU KRISTO.

Yeye ni Mungu wa Amina. Yeye habadiliki kamwe. Afanyalo halibadiliki. Analisema, na linasimama imara. Analifanya, na limekwisha milele. Hakuna anayeweza kuondoa kutoka kwenye yale Yeye asemayo wala kuongeza kwake. Na iwe hivyo. Amina. Na iwe hivyo. Hivi hamna furaha ya kwamba mnamtumikia Mungu wa namna hiyo? Unaweza kujua mahali ulipo pamoja Naye wakati wo wote na wakati wote. Yeye ni Mungu wa AMINA na hatabadilika.

*"Haya ndiyo anenayo Yeye aliye AMINA."*

Ninapenda jambo hilo. Inamaanisha ya kwamba chochote alichosema ni cha mwisho. Inamaanisha ya kwamba lo lote alilouambia ule wakati wa kwanza na ule wa pili na nyakati zote kuhusu kanisa Lake Mwenyewe lililo la kweli na alilosema kuhusu ule mzabibu wa uongo ni kweli kabisa na halitabadilika. Inamaanisha ya kwamba kile alichoanza nacho katika Mwanzo, atakimaliza katika Ufunuo. Hana budi kufanya hivyo kwa maana Yeye ni Amina, NA IWE HIVYO. Sasa tunaweza kuona tena ni kwa nini ibilisi anavichukia Vitabu vya Mwanzo na Ufunuo. Yeye anaichukia ile kweli. Yeye anajua kweli itashinda. Yeye anajua mwisho wake utakuwaje. Jinsi anavyopigana na jambo hilo. Lakini sisi tuko upande wa kushinda. Sisi (ninamaanisha waamini wa Neno Lake, peke yao) tuko upande wa Amina.

*"Haya ndiyo asemayo Shahidi aliye Mwaminifu na wa Kweli."* Sasa nataka kukuonyesha kile ninachopata katika wazo la "mwaminifu." Mnajua mara nyingi tunanena juu ya Mungu mkuu asiyebadilika, Ambaye Neno Lake halibadiliki. Nasi tunaponena juu Yake kwa njia hiyo mara nyingi tunapata mtazamo Wake ambao unamfanya aonekane hahusiki sana. Ni kama kwamba Mungu alifanya ulimwengu mzima na sheria zote zinazouhusu kisha akarudi nyuma akawa Mungu mkuu asiyehusika. Ni kama kwamba Mungu alifanya njia ya wokovu kwa ajili ya wanadamu waliopotea, njia hiyo ikiwa ni msalaba, na halafu wakati kifo cha Kristo kilipofanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, na kufufuka Kwake kukatupa mlango uliofunguliwa wa kuingia Kwake, Mungu alikunja mikono Yake tu akarudi nyuma na kusimama. Ni kama kwamba tuliweka juhudi katika kuamini Muumba Aliye mkuu, Ambaye baada ya kuumba, hakuvutiwa tena binafsi na viumbe Vyake. Sasa nasema hivyo ndivyo watu wengi mno wanavyoelekea kuwazia. Lakini hayo ni mawazo mabaya, kwa kuwa Mungu ANATAWALA KATIKA MAMBO YA WANADAMU SASA HIVI. YEYE NI MUUMBA NA MPAJI.

Wakolosai 1:16-17.

*"Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa na Yeye, na kwa ajili Yake.*

*Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika Yeye."*

Yeye ni Mungu Mwenye enzi. Kwa shauri Lake Mwenyewe Yeye alikusudia mpango wa wokovu wa wateule Wake Mwenyewe ambao aliwajua tangu zamani. Mwana alikufa msalabani apate kutengeneza njia ya Wokovu na Roho Mtakatifu anafanya mapenzi ya Baba kwa uangalifu. Yeye anatenda mambo yote wakati huu kulingana na kusudi la mapenzi Yake Mwenyewe. Yeye yuko moja kwa moja katikati ya hayo yote. Yeye yuko katikati ya kanisa Lake. Huyu Muumba mkuu, Mungu- Mwokozi anatenda kazi kwa uaminifu miongoni mwa watu Wake sasa hivi kama Mchungaji mkuu wa kondoo. Kuishi Kwake hasa ni kwa ajili ya walio Wake. Anawapenda na kuwajali. Jicho Lake daima liko juu yao. Wakati Neno linaposema ya kwamba "maisha yenu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu inamaanisha vile linavyosema hasa Loo! ninafurahi sana ya kwamba Mungu Wangu anadumu mwaminifu. Yeye ni mwaminifu Kwake Mwenyewe, hatasema uongo. Yeye ni mwaminifu kwa Neno, ataliunga mkono. Yeye ni wa kweli kwetu sisi, hatampoteza hata mmoja wetu, bali atatufufua katika siku ya mwisho. Ninafurahi ya kwamba ninapumzika katika uaminifu Wake.

Wafilipi 1:6.

*"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye Aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata Siku ya Kristo Yesu."*

*"Yeye ndiye Shahidi wa Kweli."*

Sasa neno hili, wa kweli, ni neno lile lile tulililoliona kule nyuma katika Ufu. 3:7. Mnakumbuka ya kwamba halimaanishi „kweli" iliyo kinyume cha „uongo." Lina maana yenye uzito, na yenye kilindi zaidi kwa mbali mno. Linaonyesha ujuzi mkamilifu wa jambo ukilinganisha na ujuzi wa sehemu. Sasa huko nyuma katika Wakati wa Filadelfia, kuja kwa Bwana kulikuwa kunakaribia. Ni upendo mkuu jinsi gani uliodhihirishwa ma wakati huo kwa ajili Yake.

Linanikumbusha juu ya maneno yale mazuri ya I Pet. 1:8,

*"Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona;Ambaye ijapokuwa hammwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, na yenye kujaa utukufu."*

Tunafurahi pamoja nao pia. Hatujamwona, lakini tumemhisi. Tunamjua sasa kiasi ambacho hisi zetu zenye kikomo zinaweza kuturuhusu. Lakini siku moja itakuwa uso kwa uso. Hiyo ni kwa ajili ya wakati huu. Yeye yuaja mwishoni mwa wakati huu. Ujuzi wa sehemu utafanywa UJUZI MKAMILIFU, UJUZI ULIOKAMILISHWA. Haleluya! Tumekuwa tukiona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo, lakini hivi karibuni itakuwa ni uso kwa uso. Tumekuwa tukienda toka utukufu hadi utukufu, lakini hivi karibuni itakuwa moja kwa moja katika utukufu; na TUTANG"AA katika UTUKUFU WAKE. TUTAKUWA KAMA YEYE, TUTAFANANA VYA KIAJABU SANA NAYE, YESU ALIYE MUNGU MWOKOZI WETU! Hilo si ni la ajabu? Sisi tumekamilika katika Yeye. Hiyo ni kweli. Yeye hangeweza kutudanganya kuhusu jambo hilo. Lakini siku moja tutabadilishwa katika atomi. Tutavaa kutokuharibika. Tutamezwa kabisa katika uzima. Ndipo TUTAPATA UJUZI MKAMILIFU.

*"Yeye ni Shahidi Aliye Mwaminifu na wa Kweli."*

Sasa tunafikiria juu ya neno hilo, 'shahidi.' Vema, ni kutoka kwenye neno hilo tunakopata neno „mfia imani". Biblia inanena juu ya Stefano na Antipa na wengineo kama mashahidi. Wao walikuwa wafia imani; walikuwa pia mashahidi. Yesu alikuwa mfia imani mwaminifu. Roho Mtakatifu ndiye shahidi wa jambo hilo. Roho anashuhudia jambo hilo. Ulimwengu ulimchukia Yesu. Ulimwua. Lakini Mungu alimpenda Naye alienda kwa Baba. Thibitisho ya kwamba Yeye alienda kwa Baba ni kwamba Roho Mtakatifu alikuja. Kama Yesu hangekuwa amepokewa na Baba, Roho hangekuja.

Soma katika Yohana 16:7-11.

*"Lakini Mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi Mimi niondoke; kwa maana Mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali Mimi nikienda Zangu, nitampeleka kwenu.*

*Naye akiisha kuja, Huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.*

*Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini Mimi;*

*Kwa habari ya haki, kwa sababu Mimi naenda Zangu kwa Baba, wala hamnioni tena;*

*Kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha*

*kuhukumiwa."*

*Uwepo wa Roho Mtakatifu katika ulimwengu huu badala ya Yesu kuwa hapa, unathibitisha ya kwamba Yesu alikuwa mwenye haki na alienda kwa Baba.*

Lakini pia inasema katika Yohana 14:18.

*"Sitawaacha ninyi YATIMA; naja kwenu."*

Yeye alimtuma Mfariji. ALIKUWA NDIYE HUYO MFARIJI. Alirudi katika ROHO juu ya kanisa la kweli. Yeye Ndiye SHAHIDI aliye mwaminifu na wa kweli katikati ya kanisa. Lakini siku moja Yeye atarudi katika mwili tena. Wakati huo atathibitisha basi ni nani mwenye nguvu pekee aliye na hekima,—ni Yeye, Yesu Kristo Bwana wa Utukufu.

Shahidi aliye Mwaminifu na wa Kweli, Muumba na Mpaji, Ujuzi Mkamilifu, Amina wa Mungu.

Loo! jinsi ninavyompenda, jinsi ninavyomwabudu, Yesu Mwana wa Mungu.

Nataka kumalizia mawazo yangu juu ya sehemu hii ya salamu kwa maneno haya ya

II Wakorintho 1:18-22.

*"Lakini kama Mungu alivyo mwaminifu, neno letu kwenu si ndiyo na siyo.*

*Maana Mwana wa Mungu, Kristo Yesu, aliyehubiriwa katikati yenu na sisi, yaani, mimi na Silwano na Timotheo, hakuwa ndiyo na siyo; bali katika Yeye ni ndiyo.*

*Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika Yeye ni ndiyo; tena kwa hiyo katika Yeye ni Amina; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.*

*Basi Yeye atufanyaye imara pamoja nanyi katika Kristo, na kututia mafuta, ni Mungu,*

*Naye ndiye aliyetutia muhuri akatupa arabuni ya Roho mioyoni mwetu."*

*"Mwanzo Wa Kuumba Kwa Mungu."*

Huyo ndiye Ambaye Bwana Yesu anayesema ya kwamba ni Yeye Mwenyewe. Lakini maneno hayo hayamaanishi jinsi hasa kama yanavyosikika kwetu. Kuyachukua tu jinsi yanavyosikika yamewafanya baadhi ya watu fulani (kusema kweli ni umati wa watu) kupata wazo kwamba Yesu alikuwa kiumbe cha kwanza kuumbwa na Mungu, likimfanya Yeye kuwa mdogo kuliko Mungu. Ndipo kiumbe hiki cha kwanza kikaumba ulimwengu wote mwingine na cho chote kilichomo ndani yake. Lakini hiyo si kweli. Mnajua jambo hilo haliambatani na sehemu iliyosalia ya Biblia. Maneno hayo ni, "Yeye Ndiye MWANZO ama MWANZILISHI wa kuumba kwa Mungu." Sasa tunajua kwa hakika ya kwamba Yesu ni Mungu, Mungu halisi. Yeye ndiye Muumbaji.

Yohana 1:3

*"Vyote vilifanyika kwa Huyo; wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika."*

Yeye Ndiye anayenenwa habari Zake, Mwa. 1:1

*"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."*

Pia inasema katika Kut. 20:11,

*"Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba."*

Mnaona, hapana shaka ya kwamba Yeye ndiye Muumba. Alikuwa Muumba wa UUMBAJI WA MAUMBILE YALIYOMALIZIKA.

Hakika tunaweza kuona kile ambacho maneno haya yanamaanisha sasa. Kuwa na tafsiri nyingine yo yote ingemaanisha ya kwamba Mungu alimuumba Mungu. Mungu angewezaje kuumbwa wakati Yeye, Mwenyewe, ndiye Muumba?

Lakini sasa Yeye amesimama katikati ya Kanisa. Wakati anaposimama pale akijifunua Yeye yu Nani katika wakati huu wa mwisho, Yeye anajiita "Mwanzo wa kuumba kwa Mungu." Huu ni UUMBAJI MWINGINE. Hili linahusiana na kanisa. Hii ni sifa nyingine maalum Yake Mwenyewe. Yeye ndiye MUUMBA wa kanisa hilo. Bwana arusi wa mbinguni alimuumba bibi-arusi wake. Akiwa Roho wa Mungu, alishuka na kuumba katika bikira Mariamu chembechembe ambazo kwazo mwili Wake ulizaliwa. Ninataka kurudia jambo hilo. Yeye aliumba chembechembe zenyewe katika tumbo la uzazi la Mariamu kwa ajili ya mwili huo. Haikutosha kwa Roho Mtakatifu kutia uhai kwa urahisi tu katika yai la mwanadamu lililotolewa na Mariamu. Hiyo ingekuwa ni mwanadamu mwenye dhambi akiuzaa mwili. Hilo halingeweza kumzaaa "Adamu

wa Mwisho.” Kumhusu Yesu ilisemwa “Tazama mwili Wewe (Baba) umeniwekea tayari.” Mungu (si Mariamu) ndiye aliyetoa mwili huo. Mariamu alikuwa chombo cha kibinadamu cha kuangulia naye alimbeba Mtoto Mtakatifu na akamzaa. Alikuwa Mungu-mwanadamu. Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa ni wa ule uumbaji MPYA. Mwanadamu na Mungu walikutana na kuungana; Yeye alikuwa ni wa kwanza wa jamii hii mpya. Yeye Ndiye kiongozi wa jamii hii mpya.

Wakolosai 1:18,

*“Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; Naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.”*

II Wakorintho 5:17

*“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yote yamekuwa mapya.”*

Hapo unaweza kuona ya kwamba ingawa mwanadamu alikuwa ni wa UTARATIBU ule WA KALE ama uumbaji, sasa katika KUUNGANA NA KRISTO, amekuwa KIUMBE KIPYA cha Mungu.

Waefeso 2:10,

*“Maana tu kazi Yake, TULIUMBWA KWA KUUNGANA NA KRISTO YESU tutende matendo mema.”*

Waefeso 4:24,

*“Mkavae UTU MPYA ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.”*

Huu Uumbaji Mpya si ule uumbaji wa kale uliotengenezwa tena, la sivyo haungeitwa uumbaji mpya. Hivi ndivyo hasa inavyosema ulivyo, UUMBAJI MPYA.“ Ni uumbaji mwingine, tofauti na ule wa kale. Hashughuliki tena na mambo ya mwili. Hivyo ndivyo alivyoshughulika na Israeli. Alimchagua Ibrahimu, na uzao wa Ibrahimu kwa kupitia ukoo mcha Mungu wa Isaka. Lakini sasa kutoka katika kila jamaa, kabila na taifa Yeye amekusudia kiumbe kipya. Yeye ndiye wa kwanza wa uumbaji huo. Yeye alikuwa ni Mungu aliyeumbwa kwa mfano wa mwanadamu. Sasa kwa Roho Wake Yeye anajiumbia Wana wengi Mwenyewe. Mungu muumba, akijiumba Mwenyewe sehemu ya uumbaji Wake.

Huu ndio ufunuo wa kweli wa Mungu. Hili lilikuwa ndilo kusudi Lake. Kusudi hili lilifanyika kwa kuteuliwa. Hiyo ndiyo sababu Yeye aliweza kuangalia moja kwa moja hata kwenye wakati wa mwisho wakati yote yatakuwa yamekwisha na kujiona Mwenyewe angali akiwa katikati ya kanisa, kama mwanzilishi wa huu Uumbaji Mpya wa Mungu. Nguvu za Ukuu Wake zilitimiza jambo hilo. Kwa amri Yake Mwenyewe Yeye aliwachagua washiriki wa Uumbaji huu Mpya. Aliwachagua tangu zamani wapate kufanywa wana kulingana na uradhi wa mapenzi Yake. Kwa kujua Kwake yote na kwa kuwa Kwake na nguvu zote alilitimiza. Vinginevyo angewezaje kujua kwamba angesimama katikati ya kanisa akipokea utukufu kutoka kwa ndugu Zake kama Yeye hakuhakikisha? Alijua mambo yote, na alitenda mambo yote kulingana na yale aliyojua ili kwamba kusudi Lake na uradhi wa mapenzi Yake vitimizwe.

Waefeso 2:11

*“Ndani Yake sisi nasi tulifanywa warithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi Lake Yeye ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi Yake.”*

Haleluya! Hivi huna furaha kwamba wewe ni mali Yake!

**UJUMBE KWA WAKATI WA LAODIKIA**

Ufunuo 3:15-19

*“Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto.*

*Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu.*

*Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.*

*Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, na kwamba aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*

*Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.“*

Tulipokuwa tunasoma hili pamoja nina hakika ya kwamba umeona ya kwamba Roho hajasema jambo moja zuri kuhusu wakati huu. Yeye anatoa mashtaka mawili na kutoa hukumu Yake juu ya mashtaka hayo.

**(1) Ufunuo 3:15,16**

*"Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto;*

*Ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu."*

Tutachunguza jambo hili kwa makini. Inasema ya kwamba kundi hili la wakati huu wa kanisa la Laodikia ni vuguvugu. Uvuguvugu huu unastahili hukumu kutoka kwa Mungu. Hukumu ni kwamba wao watatapikwa watoke katika kinywa Chake. Hapa ndipo hatutaki kukosea kama watu wengi wanavyofanya. Wao wanasema pasipo busara kabisa ya kwamba Mungu anaweza kukutapika utoke katika kinywa Chake na hilo linathibitisha ya kwamba hakuna kitu kama ukweli wo wote kwenye fundisho la uvumilivu wa Watakatifu. Ninataka kusahihisha mawazo yako sasa hivi. Aya hii haitolewi kwa mtu binafsi. Inapewa kanisa. Yeye analizungumzia kanisa. Isitoshe, kama utaliweka tu Neno niani utakumbuka ya kwamba hakuna mahali linaposema ya kwamba sisi tuko katika KINYWA cha Mungu. Tumechorwa kwenye vitanga vya mikono Yake. Tumebebwa moyoni Mwake. Huko nyuma kabisa katika nyakati zisizojulikana kabla ya wakati tulikuwa katika nia Yake. Tuko katika zizi Lake, na katika malisho Yake, lakini kamwe si katika kinywa Chake. Lakini ni kitu gani kilicho katika kinywa cha Bwana? Neno liko kinywani Mwake.

Mathayo 4:4

*"Lakini akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."*

Neno linapaswa kuwa vinywani mwetu, pia. Sasa tunajua ya kwamba kanisa ni mwili Wake. Liko hapa likipachukua mahali Pake. Ni kitu gani kitakachokuwa kinywani mwa kanisa? NENO.

I Petro 4:11

*"Mtu akisema, na aseme kama mausia (Neno) ya Mungu."*

II Petro 1:21

*"Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali watu watakatifu wa Mungu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu."*

Basi watu hawa wa siku za mwisho wana shida gani? WAMEONDOKA KWENYE NENO. HAWANA MOTO TENA KUHUSU HILO. WAO NI VUGUVUGU KUHUSU HILO. Nitathibitisha jambo hilo sasa hivi.

Wabatisti wana kanuni zao za imani na mafundisho ya sharti yaliyo na msingi wake katika Neno nawe huwezi kuwatikisa. Wao wanasema siku za miujiza za mitume zimekwisha na hakuna Ubatizo wa Roho Mtakatifu, baada ya kuamini. Wamethodisti wanasema (kwa kutumia Neno) hakuna ubatizo wa maji (kunyunyizia si ubatizo) na ya kwamba utakaso ndio Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kanisa la Kristo linashikilia sana ubatizo wa kuzaliwa mara ya pili na mara nyingi sana wanatumbukizwa wakiwa wenye dhambi wakavu na kutoka wakiwa wenye dhambi waliolowa maji. Hata hivyo wao wanadai ya kwamba mafundisho yao yana msingi wake katika Neno. Nenda moja kwa moja kwenye mstari na uwafikie Wapentekoste. Je! Wana Neno? Wape jaribio la Neno uone. Wao wataliuza Neno kwa jambo la kusisimua karibu kila wakati tu. Kama unaweza kutoa madhihirisho kama mafuta na damu na lugha na ishara nyinginezo, kama ziko kwenye Neno ama haziko, ama kama hayo yamefasiriwa vizuri kutoka kwenye Neno, walio wengi watalikimbilia. Lakini ni nini kimelipata Neno? Neno limewekwa kando, kwa hiyo Mungu anasema, "Mimi niko kinyume nanyi nyote. Nitawatapika mtoke katika kinywa Changu. Huu ndio mwisho. Kwa kuwa saba kati ya nyakati saba, sijaona kitu ila watu wakiliheshimu neno lao wenyewe kuliko Langu. Kwa hiyo mwishoni mwa wakati huu ninawatapika mtoke katika kinywa Changu. Yote yamekwisha. Nitazungumza basi. Naam, niko hapa katikati ya Kanisa. Amina wa Mungu, aliye mwaminifu na wa kweli atajifunua Mwenyewe na itakuwa KWA NJIA YA NABII WANGU." Naam, hivyo ndivyo ilivyo.

Ufunuo 10:7

*"Na katika siku za sauti ya mjumbe wa saba, atakapoanza kupiga baragumu, siri ya Mungu itatimizwa kama alivyowahubiri watumishi Wake manabii."*

Hilo hapo. Yeye anamtuma nabii aliyethibitishwa. Anatuma nabii baada ya karibu miaka elfu mbili. Yeye anamtuma mtu fulani aliye mbali sana na madhehebu, elimu, na ulimwengu wa dini hivi kwamba kama vile Yohana Mbatizaji na Eliya wa kale, yeye atasikia tu kutoka kwa Mungu na atakuwa na "Bwana asema hivi" na kunena kwa niaba ya Mungu. Yeye atakuwa kinywa cha Mungu NAYE, KAMA

INAVYOTANGAZWA KATIKA MAL. 4:6, ATAIGEUZA MIOYO WA WATOTO IWAELEKEE BABA ZAO. Atawarudisha wateule wa siku za mwisho nao watamsikiliza nabii aliyethibitishwa akitoa kweli halisi kama vile ilivyokuwa kwa Paulo. Atairudisha kweli kama walivyokuwa nayo. Na hao wateule walio pamoja naye katika siku hiyo watakuwa ndio wanaomdhihirisha Bwana kwa kweli na watakuwa ndio Mwili Wake na kuwa sauti Yake na kutenda kazi Zake. Haleluya! Mnaona jambo hilo?

Kuzingatiwa kwa muda mfupi kwa historia ya kanisa kutathibitisha jinsi wazo hili lilivyo sahihi. Katika Zama za Giza watu walikuwa karibu wamepotelewa na Neno. Lakini Mungu alimtuma Luther akiwa na NENO. Waluteri walikuwa ni kinywa cha Mungu kwa wakati huo. Lakini wao wakaunda madhehebu, na tena hilo Neno safi lilipotezwa kwa maana madhehebu huegemea kwenye mafundisho ya sharti na kanuni za imani, wala hawaegemei kwenye Neno lililo halisi. Wao hawakuweza tena kuwa kinywa cha Mungu. Ndipo Mungu akamtuma Wesley, naye alikuwa ndiye sauti iliyokuwa na Neno katika siku yake. Watu waliouchukua ufunuo wake kutoka kwa Mungu wakawa nyaraka zilizo hai zilizosomwa na kujulikana na watu wote kwa ajili ya kizazi chao. Wakati Wamethodisti waliposhindwa, Mungu aliwainua wengine na kwa hiyo jambo hilo limeendelea kwa miaka mingi mpaka katika wakati huu wa mwisho kuna watu wengine nchini, ambao chini ya mjumbe wao watakuwa ndio sauti ya mwisho kwa wakati wa mwisho.

Naam bwana. Kanisa si "kinywa" cha Mungu tena. Ni kinywa chake lenyewe. Kwa hiyo Mungu analiacha. Ataliangamiza kupitia kwa nabii na bibi-arusi, kwa kuwa sauti ya Mungu itakuwa ndani ya bibi-arusi.

Naam iko, kwa maana inasema katika sura ya mwisho ya Ufu. aya ya 17

> *"Roho na bibi-arusi wasema, njoo."*

Mara nyingine tena ulimwengu utasikia moja kwa moja kutoka kwa Mungu kama ilivyokuwa wakati wa Pentekoste; lakini bila shaka huyo Bibi-arusi Neno atakataliwa kama ilivyokuwa katika wakati wa kwanza.

Sasa Yeye ameupigia kelele wakati huu wa mwisho, "Mnalo Neno. Mna Biblia nyingi kuliko mlivyowahi kuwa, lakini hamfanyi lo lote juu ya Neno ila kuligawanya na kulipasua vipande-vipande, mkichukua mnalotaka na kuacha yale msiyotaka. Hamtaki KULIISHI, ila kulibishania. Afadhali mngalikuwa baridi ama moto. Kama mngalikuwa baridi na mkalikataa, ningaliweza kuvumilia jambo hilo. Kama mngalikuwa moto kweli kweli kujua ni kweli na kuliishi, ningewasifu kwa ajili ya jambo hilo. Lakini wakati mnapolichukua tu Neno Langu wala hamliheshimu, Mimi Nami sina budi kukataa kuwaheshimu. Nitawatapika kwa maana mnanichefua moyo."

Sasa mtu ye yote anajua ya kwamba maji yenye uvuguvugu ndiyo yanayokuchefua moyo. Kama unataka dawa ya kutapisha, maji yenye uvuguvugu ndiyo yanayofaa sana kunywa. Kanisa vuguvugu limemchosha Mungu Naye ametangaza atalitapika. Inatukumbusha jinsi alivyojisikia kabla tu ya ile gharika, sivyo?

Ee Mungu! laiti kanisa lingalikuwa baridi ama moto. Ni afadhali sana, lingekuwa na juhudi (moto). Lakini si moto. Hukumu imetolewa. Yeye si sauti ya Mungu tena kwa ulimwengu. Litashikilia kwamba ndivyo lilivyo, lakini Mungu anasema sivyo.

Loo! Mungu yungali ana sauti kwa ajili ya watu wa ulimwengu, kama vile tu aliyompa bibi-arusi sauti. Sauti hiyo imo ndani ya bibi-arusi kama tulivyosema na tutazungumza zaidi juu ya jambo hilo baadaye.

**(2) Ufunuo 3:17-18,**

> *"Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.*
>
> *Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyojaribiwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."*

Sasa angalia fungu la kwanza la maneno ya aya hii, "kwa kuwa wasema." Mnaona, wao walikuwa wananena. Walikuwa wakinena kama kinywa cha Mungu. Hili linathibitisha yale hasa niliyosema aya za 16-17 zilichomaanisha. Lakini ingawa wao wanasema hivyo, hilo halilifanyi kuwa ni sawa. Kanisa Katoliki linasema ya kwamba linanena kwa niaba ya Mungu, likisema ndilo sauti ya hakika ya Bwana. Jinsi watu wo wote wanavyoweza kuwa waovu kiroho jinsi hiyo ni zaidi ya nijuavyo mimi, lakini wao wanazaa kulingana na mbegu iliyo ndani yao, nasi tunajua mahali mbegu hiyo ilikotoka, sivyo?

Kanisa la Laodikia linasema, "Mimi ni tajiri na nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu." Hivyo ndivyo lilivyojipima. Lilijiangalia na hilo ndilo lililoona. Likasema, "Mimi ni tajiri," ambalo linamaanisha ni tajiri katika mambo ya ulimwengu huu.

Linajigamba mbele ya Yakobo 2:5-7,

*"Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni, Je! Mungu hakuwachagua maskini wa dunia hii wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao? Bali ninyi mmemvunjia heshima maskini.*

*Je! matajiri hawawaonei ninyi na kuwavuta mbele ya viti vya hukumu?*

*Hawalitukani Jina lile zuri mliloitwa?"*

Sasa mimi SIDOKEZI ya kwamba tajiri hawezi kuwa wa Kiroho, bali sote tunajua ya kwamba Neno linasema ni wachache sana walio wa kiroho. Maskini ndio walio wengi katika mwili wa kanisa la kweli. Sasa basi, kama kanisa likijaa mali, tunajua jambo moja tu; "Ichabod" limeandikwa kwenye malango yake makubwa! Huwezi kukana hilo, kwa maana hilo ni Neno.

Nena kuhusu mali kanisani—mbona kamwe hakujakuweko na onyesho kama hilo la mali. Madhabahu nzuri zimeongezeka kuliko isivyopata kuwa hapo awali. Makundi mbalimbali yanashindana wao kwa wao kuona ni nani anaweza kujenga yaliyo makubwa na mazuri kuliko yote. Nao wanajenga vituo vya elimu vinavyogharimu mamilioni yasiyokisika, na majengo hayo yanatumiwa tu kwa saa moja ama mawili kwa juma. Sasa jambo hilo halingekuwa baya sana, lakini wanatarajia wakati huu mdogo unaotumiwa na watoto kwenye kituo hicho cha elimu kupachukua mahali pa masaa ya kufundishwa yanayopaswa kutolewa nyumbani.

Pesa zimemwagwa kanisani hata madhehebu mbalimbali yana rasilmali na dhamana, viwanda, mashimo ya mafuta, na makampuni ya bima. Wamemwaga pesa katika ustawi wa jamii na kwenye hazina za kustaafu. Sasa hili linasikika kwamba ni zuri, lakini limekuwa mtego kwa wahudumu, kwa maana kama wakiamua kuliacha kundi lao kwa ajili ya nuru zaidi ama kumpenda Mungu, wanapoteza ujira wao wa kustaafu. Walio wengi hawawezi kustahimili jambo hili nao wanakaa na kundi lao linalowabana.

Sasa msisahau ya kwamba huu ndio wakati wa mwisho. Tunajua ya kwamba huu ndio wakati wa mwisho kwa sababu Israeli wamerudi Palestina. Kama tunaamini ya kwamba Yeye kweli yuaja, basi hapana budi kuna kasoro kwa wale wanaojenga sana. Inamfanya mtu kufikiria ya kwamba watu hawa wanakusudia kukaa hapa milele, ama ya kwamba kuja kwa Yesu ni mamia ya miaka ijayo.

Unajua ya kwamba dini leo inajulikana kama biashara kubwa? Ni kweli kabisa ya kwamba wanaweka mameneja wa biashara katika makanisa washughulikie mambo ya fedha. Je! Hivi ndivyo Mungu anavyotaka? Je! Neno Lake halikutufundisha katika Kitabu cha Matendo ya kwamba watu saba waliojaa Roho Mtakatifu na imani walimtumikia Bwana katika mambo ya biashara? Hakika unaweza kuona ni kwa nini Mungu alisema, "WEWE unasema u tajiri; Mimi sikusema hivyo kamwe."

Kuna vipindi vya redio, vipindi vya televisheni, na jitihada nyingi za kanisa ambazo zinagharimu mamilioni na mamilioni ya dola. Utajiri unamiminika na kumiminika kanisani, wafuasi wanaongezeka pamoja na pesa, hata hivyo kazi haifanywi kama ilivyokuwa ikifanyika wakati hapakuwepo na pesa, lakini watu walitegemea uwezo pekee waliopewa na Roho Mtakatifu.

Kuna wahubiri wa kuajiriwa, wasaidizi wa kuajiriwa, wahudumu wa muziki na elimu wa kuajiriwa, kwaya za kuajiriwa, wasimamizi wa kuajiriwa, vipindi, na mambo ya kujifurahisha—yote yakigharimu fedha nyingi mno, lakini pamoja na hayo yote, nguvu zinapungua. Naam, kanisa ni tajiri, lakini nguvu hazipo. Mungu hutenda kazi kwa Roho Wake, si kwa kiasi cha pesa ama kipaji kanisani.

Sasa nataka kuwonyesha jinsi tamaa hii ya pesa ilivyokuwa ya kuchukiza. Makanisa yote yamejitahidi sana kupata wafuasi, hasa sana wale walio matajiri. Kila mahali kuna kilio cha kuifanya dini kuwa ya kuvutia sana na ya kupendeza kusudi matajiri na watu wastaarabu na wote walio na sifa za kilimwengu waje na kuwajibika kanisani. Je! hawawezi kufahamu ya kwamba kama utajiri ndio kipimo cha kuwa wa kiroho, basi ulimwengu tayari una Mungu, una Mungu mzima, na kanisa halina kitu?

*"Unasema nimejitajirisha."*

*Hii kihalisi inamaanisha „Nina utajiri wa Kiroho."* Hii inasikika kama ule utawala wa miaka elfu pamoja na barabara za dhahabu na uwepo wa Mungu. Lakini nashangaa kama hivi ndivyo ilivyo. Je! kanisa kweli ni tajiri kwa mambo ya Kiroho ya Mungu? Hebu na tuchunguze majivuno haya ya Laodikia ya Karne ya Ishirini katika nuru ya Neno.

Kama kanisa kweli lingekuwa tajiri Kiroho, ushawishi wake ungeenea kwenye maisha ya jamii. Lakini ni maisha ya namna gani hasa hawa wanaoitwa ni watu wa kiroho na wenye ushawishi wanayoishi? Huko nje kwenye vitongoji vya miji, huko nje kwenye mitaa ya watu wa tabaka bora, kumejaa kubadilishana wake, umalaya, na makundi ya watoto wahalifu, wakisababisha uhalifu mkubwa sana wa mali. Ufisadi umefikia kiwango cha juu sana cha nyakati zote katika matendo ya kujuana kimwili ovyo ovyo, madawa ya kulevya, kucheza kamari, kuiba, na kila namna ya uovu. Na kanisa linaendelea kudai jinsi kizazi hiki kilivyo kizuri, jinsi makanisa yalivyojaa na jinsi hata wananchi wanavyoitikia wito wa wamishenari katika nchi za ng"ambo. Kanisa limewapeleka watu kwa madaktari, hasa sana madaktari wa akili. Jinsi

linavyoweza kujigamba kuhusu kuwa tajiri Kiroho ni zaidi ya nijuavyo mimi. Si kweli. Wamefilisika na hawajui.

Angalia vizuri kila upande hapo wewe ulipo. Wachunguze watu wanapopita karibu na wewe. Katika umati unaouona, je! unaweza kuwachagua hao wanaoonekana kuwa ni Wakristo? Angalia jinsi wanavyovalia, angalia jinsi wanavyoenenda, sikia wanayosema, angalia wanakoenda. Kweli kunapaswa kuwako na ushuhuda halisi wa kuzaliwa upya kati ya hao wote tunaowaona wakipita. Lakini ni wachache. Hata hivyo leo makanisa ya kikanuni yanatwambia wana mamilioni waliookolewa na hata kujazwa na Roho. Kujazwa na Roho? Unaweza kusema wanawake wanaokwenda huko na huko na nywele zilizosokotwa na zilizokatwa, wamevaa kaptura ndefu na suruali zinazopwaya, blauzi kifuawazi na kaptura, wamejipodoa kabisa kama Yezebeli wamejazwa na Roho? Kama hawa wamevaa mavazi ya kujisetiri kama iwapasavyo wanawake Wakristo, ningechukia kufikiria jinsi ingekuwa kama ingenibidi kushuhudia onyesho la ukosefu wa adabu.

Sasa ninajua ya kwamba wanawake hao sio wanaounda hiyo mitindo. Hollywood ndiyo inayofanya jambo hilo. Lakini sikilizeni enyi mabibi, wangali wanauza vitambaa na macherehani. Si lazima ununue za madukani halafu utumie jambo hilo kama udhuru. Hili ni jambo zito sana ninaloingilia. Hujasoma katika Maandiko ya kwamba wakati mwanamume anapomtazama mwanamke na kumtamani moyoni mwake, tayari amezini naye moyoni mwake? Vipi kama ulivalia hivi kwamba ulisababisha jambo hilo? Hilo linakufanya wewe kuwa mwenzi wake katika dhambi, hata ingawa ungekuwa huna habari na jambo hilo katakata, ukiwa wewe ni bikira kweli asiye na tamaa kama hizo. Hata hivyo Mungu anakushikilia kuwa unawajibika na utahukumiwa.

Sasa ninajua ya kwamba ninyi akina mama hamtaki mahubiri ya namna hii, lakini ewe dada, umekosea kabisa katika yale ufanyayo. Biblia inakukataza kukata nywele zako. Mungu alikupa hizo ziwe badala ya mavazi. Alikuamuru uziache ziwe ndefu. Ni utukufu wako. Ulipokata nywele zako ulionyesha ya kwamba umeacha uongozi wa mume wako. Kama vile Hawa ulitoka ukaziendea njia zako mwenyewe. Mlipata haki ya kupiga kura. Mmeingilia kazi za wanaume. Mkaacha kuwa wanawake. Mnapaswa kutubu na kumrudia Mungu. Na kama mambo haya yote hayakuwa mabaya vya kutosha, wengi wenu mlichukua wazo kwamba mngeweza kuzivamia mimbara na huduma za kanisa ambazo Mungu ameziweka kwa ajili ya wanaume na wanaume peke yao. Loo! nimetonesha kidonda basi sivyo? Vema, nionyesheni mahali pamoja katika Biblia ambapo Mungu aliwahi kumchagua mwanamke ye yote kuhubiri ama kutwaa mamlaka juu ya mwanamume, nami nitaomba msamaha kwa yale niliyosema. Hamwezi kupata kwamba nimekosea. Ninasema kweli, kwa maana ninashikilia Neno na niko kwenye Neno. Kama mngalikuwa tajiri Kiroho mngejua ya kwamba hiyo ni kweli. Hakuna kweli ila Neno. Paulo alisema, "Simruhusu mwanamke kufundisha wala kumtawala mwanamume." Huwezi kamwe kuchukua nafasi katika zile huduma tano za Efe. 4 bila kuwatawala wanaume. Dada, afadhali ulisikilize hilo Neno. Haikuwa ni Roho wa Mungu akijidhihirisha katika maisha yaliyojazwa Roho aliyekwambia uhubiri kwa sababu Roho na Neno ni MMOJA. Wanasema jambo lile lile. Mtu fulani alifanya kosa. Mtu fulani alidanganywa. Amkeni kabla ya kuchelewa sana. Shetani alimdanganya Hawa, mama yako; anawadanganya binti zake sasa. Mungu na awasaidie.

*"Sina haja ya kitu."*

Sasa wakati mtu ye yote anaposema, "Sina haja ya kitu," angeweza kuwa anasema kabisa, "Nina kila kitu", ama angeweza kuwa anasema, "Sitaki mengine zaidi kwa maana nimeshiba sasa." Unaweza kutamka jambo hili kwa njia yo yote utakayo, na jumla ya yote ni kwamba kanisa limejikinai. Limeridhika na yale liliyo nayo. Aidha linawazia kwamba lina yote ama lina ya kutosha. Na hilo ndilo hasa tunalopata leo. Ni madhehebu gani yasiyodai ya kwamba YENYEWE yana ufunuo na nguvu na kweli? Wasikilizeni Wabaptisti, nao wana yote. Wasikilizeni Wamethodisti, nao wana yote. Wasikilizeni wa Kanisa la Kristo na kila mtu amekosea isipokuwa wao. Sikiliza wanayosema Wapentekoste nao wana utimilifu wa utimilifu. Sasa wao wanajua ninasema kweli juu yao, kwa maana hakuna kimoja cha vitabu vyao vya mafundisho kinachosema tofauti yo yote Waliviandika vyote vizuri sana na kuandika majina yao humo na kumaliza kila kitu. Mungu hana kitu kingine chochote zaidi. Na kuna wale ambao kweli hawataki mengine tena. Hawaamini katika kuponya wala wasingekutaka, ingawa kupo katika Neno. Kuna wale ambao hawangemkubali Roho Mtakatifu kama Mungu angalifungua mbingu na kuwaonesha ishara.

Sasa wote wanasema, na kujaribu kuthibitisha ya kwamba wana yote, ama wana ya kutosha. Hata hivyo je, hiyo ni kweli? Linganisha kanisa hili la karne ya ishirini na kanisa la karne ya kwanza. Endelea. Fanya hivyo. Nguvu ziko wapi? Upendo uko wapi? Liko wapi kanisa lililotakaswa ambalo lilihimili dhambi na kutembea kwa imani kumwelekea Yesu? Uko wapi umoja? Huwezi kuupata. Kama kanisa hili lina yote linalohitaji, mbona walikuwa wanalia wampate Mungu zaidi katika Kitabu cha Matendo kama kwamba wao hawakuwa na yote hayo, na walakini walikuwa na mambo mengi ya Mungu kuliko walivyo nayo leo?

**TIBA YA MUNGU**

Sasa yale Mungu aliyoona yalikuwa tofauti kabisa na yale waliyosema waliona. Wao walisema ya kwamba walikuwa wamejitajirisha na ni matajiri Kiroho. Walikuwa wamefika. Hawakuhitaji cho chote.

Lakini Mungu aliona vinginevyo. Alisema, "Hamjui jambo hili, lakini ninyi ni wanyonge, wenye mashaka, maskini, vipofu, na uchi." Sasa wakati watu wako hivyo, hasa sana uchi na HAWAJUI, hapana budi kuwe na jambo fulani baya sana. Hakika hapana budi jambo fulani linatendeka. Si kwamba Mungu amepofusha macho yao kama alivyowafanyia Wayahudi? Je! Injili inawarudia Wayahudi? Je! Historia inajirudia? Nasema ndivyo ilivyo.

Mungu anasema kanisa hili la Wakati wa Laodikia ni "nyonge". Neno hilo linatokana na maneno mawili ya Kiyunani ambayo yanamaanisha 'kuvumilia' na 'kujaribiwa.' Na halina uhusiano wo wote na majaribu yanayompata Mkristo wa kweli kwa maana Mungu anamwelezea Mkristo aliye katika majaribu kama "aliyebarikiwa" na mwelekeo wake ni wa furaha ambapo maelezo haya yametajwa kama "mnyonge na mwenye mashaka". Ni ajabu iliyoje. Katika wakati huu wa wingi, katika wakati huu wa maendeleo, katika wakati huu wa vitu tele, kunawezaje kuweko na majaribu? Vema sasa, ni ajabu; lakini katika wakati huu wa wingi na ufaao, wakati kila mtu ana mengi sana na kuna mengi sana ya kupatikana, vipi tukiwa na vyombo vyote vilivyovumbuliwa kufanya kazi zetu na vitu vingi sana vya kutufurahisha, MARA, tunaona ugonjwa wa akili ukienea sana hata unalitia hofu taifa. Ambapo kila mtu anapaswa kuwa na furaha, bila ya kuwa na kitu kwa kweli cha kumfanya mtu kutokuwa na furaha, mamilioni wanakunywa dawa za kutuliza ubongo usiku, madawa ya kuwachangamsha asubuhi, wakikimbilia kwa madaktari, wakiingia mahospitalini, na kujaribu kunyamazisha hofu zisizojulikana kwa pombe.

Naam, wakati huu unajivunia maghala yake makubwa mno ya bidhaa za ulimwengu, lakini watu wamepungukiwa na furaha kuliko walivyowahi kuwa. Wakati huu unajivunia mafanikio yake ya kiroho, lakini watu hawajiamini kuliko walivyowahi kujiamini. Wakati huu unajivunia maadili bora zaidi na umepotoka zaidi kuliko wakati wo wote tangu ile gharika. Unazungumzia juu ya maarifa yake na sayansi, lakini unapigana vita unavyoshindwa katika fani zote, kwa kuwa akili ya mwanadamu na nafsi na roho haviwezi kufahamu ama kwenda sambamba na mabadiliko yote ambayo yamekuja juu ya nchi. Katika kizazi kimoja tumeenda mbali kutoka kwenye wakati wa mkokoteni wa farasi kuingia kwenye wakati wa wanaanga, nasi tunajivunia na kujigamba juu ya jambo hilo; lakini mle ndani kuna shimo tupu lenye giza linalolia kwa mateso, na BILA SABABU YO YOTE INAYOJULIKANA mioyo ya wanadamu inavunjika kwa hofu na ulimwengu una giza sana hivi kwamba wakati huu ungeweza kuitwa wakati wa wenda wazimu. Unajivuna, lakini hauwezi kudhihirisha jambo hilo. Unapigia shime amani, wala hakuna amani. Unasema kwa sauti kuu ya kwamba una wingi wa mambo yote, lakini unaendelea kuwaka tamaa kama moto usioridhika! "Hakuna amani", Mungu wangu awaambia waovu.

*"Wao ni wenye mashaka."* Hiyo ina maana kwamba wao ni watu wa kusikitikiwa. Ati kusikitikiwa? Wao wanapuuza kusikitikiwa. Wamejaa kiburi. Wanajivunia waliyo nayo. Lakini waliyo nayo hayatastahimili jaribio la wakati. Wamejenga juu ya mchanga wa kudidimiza badala ya mwamba wa ufunuo wa Neno la Mungu. Hivi karibuni tetemeko la nchi linakuja. Hivi karibuni kutakuja dhoruba za hasira ya Mungu katika hukumu. Ndipo yatakuja maangamizi ya ghafla, na licha ya matayarisho yao yote ya kimwili watakuwa bado hawajajitayarisha kwa yale yatakayokuja juu ya nchi. Hao ndio wale ambao mbali na jitihada zao zote za ulimwengu kweli wanajipinga wenyewe na hawajui. Kweli wao ni watu wa kusikitikiwa. Wasikitikie watu maskini walio katika pilikapilika hizi za ekumeni za siku ya mwisho kwa kuwa wanasema jambo hilo kwamba ni la Mungu, ambapo ni la Shetani. Wasikitikie hao wasiojua laana ya madhehebu. Wasikitikie hao walio na makanisa mengi sana mazuri, nyumba nzuri namna hiyo za makasisi, kwaya nzuri sana zilizofunzwa, onyesho kubwa sana la utajiri na namna ya kuabudu iliyo tulivu na yenye uchaji namna hiyo. Wasikitikie, usiwaonee wivu. Rudini kwenye majengo ya maghala ya kale, rudini kwenye vyumba visivyo na mwangaza wa kutosha, rudini kwenye vyumba vidogo vya chini, rudini kwenye machache ya ulimwengu na mengi ya Mungu. Wahurumie wale wanaofanya madai yao makubwa, na kuzungumzia vipawa vyao. Wahurumieni kama vyombo vya kusikitikiwa, kwa maana siku si nyingi watakuwa vyombo vya hasira.

*"Wao ni maskini."* Sasa bila shaka hilo linamaanisha maskini Kiroho. Ishara ya wakati huu unapomalizika, ni makanisa makubwa na bora zaidi, yakizidi kujaa watu, yakizidi kuwa na madhihirisho ya yale yanayodhaniwa kuwa ni madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Lakini madhabahu zilizojaa, karama za Roho zikitenda kazi, kuhudhuria kuzuri sana si jibu kutoka kwa Mungu, kwa maana hao wanaokuja madhabahuni ni kwa shida sana wao hubaki wapate kuendelea na Mungu, na baada ya zile kampeni kuu kumalizika, wako wapi hao wote walioshuka wakaja kupitia kwenye nafasi za kupitia za marefu ya kanisa? Walimsikiliza mwanadamu, walisikiliza wito, waliingia katika jarife, lakini hawakuwa samaki, na kama vile kasa walitambaa wakarudi kwenye maji yao wenyewe.

Halafu kuna mazungumzo haya yote kuhusu glosalalia_ inadhaniwa kuwa ndio ushuhuda wa Ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao watu wanadhani ya kwamba tuko katikati ya ufufuo mkuu. Uamsho umekwisha. Marekani ilikuwa na nafasi yake ya mwisho mnamo 1957. Sasa lugha ni ishara ya Mungu ya maangamizi yajayo, kama vile ilivyokuwa wakati zilipotokea ukutani kwenye karamu ya Belshaza. Hamjui ya kwamba wengi watatokea katika siku ya mwisho na kusema, "Bwana, Bwana, je! hatujafanya kazi nyingi za ajabu katika Jina Lako, hata kutoa pepo?

Naye atasema,

*"Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwajua kamwe."*

Mathayo 7:22-23.

Yesu alisema walikuwa watenda maovu. Hata hivyo, unampata mtu anayeweza kuja na kuwaombea wagonjwa, anafanya mafuta na damu kutokea kwenye kusanyiko, unabii unatoka na kila namna ya mambo ya kimbinguni, nao watu watamzunguka, na kuapa ya kwamba yeye ni wa Bwana, hata ingawa yeye anafanya dini kuwa njama za kupata fedha na kuishi katika dhambi. Jibu pekee walilo nalo ni jibu lisilo la kibiblia katakata la "vema, yeye anapata matokeo, kwa hiyo hana budi kuwa ni wa Mungu." Ni jambo la kutisha iliyoje. Jinsi wakati huu ulivyo maskini kweli katika Roho wa Mungu, na hao maskini wasio na kitu wala hawajui.

*"Wewe ni kipofu na uchi."* Sasa hili kweli ni jambo la kukatisha tamaa. Mtu yeyote anawezaje kuwa kipofu na uchi na asijue jambo hilo? Hata hivyo inasema ya kwamba wao ni vipofu na uchi wala hawawezi kujua jambo hilo. Jawabu ni, wao ni vipofu kiroho, na uchi kiroho. Unakumbuka wakati Elisha na Gehazi walipozungukwa na jeshi la Washami? Mnakumbuka ya kwamba Elisha aliwapofusha kwa nguvu za Mungu. Hata hivyo macho yao yalikuwa yamefunguliwa na wangeweza kuona mahali walipokuwa wakienda. Huo upofu ulikuwa ni wa ajabu kwa vile wao waliweza kuona mambo fulani, lakini mambo fulani mengine kama vile Elisha na mtumishi wake na kambi ya Israeli hawakuweza kuona. Yale jeshi hili lilichoweza kuona hakingeweza kuwasaidia. Yale wasiyoweza kuona ndiyo yaliyosababisha kuchukuliwa kwao mateka. Sasa hili lina maana gani kwetu? Linamaanisha jinsi hasa lilivyomaanisha kule nyuma katika huduma ya duniani ya Yesu. Yeye alijaribu kuwafundisha kweli, lakini wasingesikiliza.

Yohana 9:40-41.

> *"Baadhi ya Mafarisayo waliokuwepo pamoja naye wakasikia hayo, wakamwambia, Je! sisi nasi tu vipofu?*
>
> *Yesu akawaambia, Kama mngekuwa vipofu, msingekuwa na dhambi; lakini sasa mwasema, Twaona; basi dhambi yenu inakaa."*
>
> Tabia ya wakati huu ni kama vile kabisa ilivyokuwa wakati ule. *Watu wana kila kitu. Wanajua yote. Hawafundishwi na mtu. Kama jambo la kweli katika Neno likitokea na mtu fulani anajaribu kueleza maoni yake kwa mtu aliye na mawazo tofauti, anayesikiliza hasikilizi hata kidogo kusudi apate kujua, lakini anasikiliza tu apate kukanusha yale yanayosemwa. Sasa nataka kuwaulizeni swali zuri. Maandiko yanaweza kupingana na Maandiko? Je! Biblia inapingana na Biblia? Kunaweza kuwe na mafundisho mawili ya kweli katika Neno yanayosema kinyume ama yanayopingana? LA. HAIWEZEKANI. Hata hivyo ni watu wa Mungu wangapi wamefungua macho yao kwa ajili ya kweli hiyo? Si hata moja kwa mia, nijuavyo mimi, wamejua ya kwamba Maandiko YOTE yametolewa na Mungu na YOTE yanafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwasahihisha, nk. Kama Maandiko yote yametolewa namna hiyo, basi kila aya itaambatana na nyingine ikipewa nafasi. Lakini ni wangapi wanaoamini katika kuchaguliwa tangu zamani kwa ajili ya kuteuliwa na kukataliwa kwa ajili ya kuangamizwa? Hao ambao hawaamini, je! watasikiliza? La, hawatasikiliza. Hata hivyo wote wawili wamo katika Neno, wala hakuna kitu kitakacholibadilisha. Lakini kujua jambo hilo na kupatanisha kweli ya mafundisho hayo pamoja na kweli nyingine ambazo zinaonekana kama zinapinga, hawana muda. Lakini wao huziba masikio yao, na kusaga meno yao, na wanapata hasara. Katika mwisho wa wakati huu nabii atakuja, bali wao watakuwa vipofu kwa yale yote anayofanya na kusema. Wao wana uhakika sana wako sawa, na katika upofu wao watapoteza yote.*

Sasa Mungu anasema wako uchi na pia ni vipofu. Siwezi kuwazia jambo lo lote la huzuni kama mtu ambaye ni kipofu na yu uchi naye hajui. Kuna jibu moja tu—amerukwa na akili. Yeye tayari yuko ndani kabisa ya usahaulifu. Akili zake zimepotea, usahaulifu wa kiroho umeingia. Linaweza kumaanisha nini tena? Linaweza kumaanisha ya kwamba Roho Mtakatifu ameliacha kanisa hili la siku za mwisho? Linaweza kumaanisha ya kwamba watu wamemsahau Mungu mioyoni mwao kiasi kwamba inatukia kama vile ilivyoandikwa katika Rum. 1:28.

> *"Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa."*

Hakika inaonekana ya kwamba jambo kama hilo limetukia. Hawa hapa watu wanaosema ya kwamba wao ni wa Mungu na wanamjua Mungu na wana Roho Wake Mtakatifu, na hata hivyo wao ni uchi na vipofu wala hawajui. Wao TAYARI WAMEDANGANYIKA. WANA ROHO MBAYA. WATEULE HAWAWEZI KUDANGANYWA, LAKINI NI DHAHIRI YA KWAMBA HAWA WENGINE WAMEDANGANYWA. Hawa ndio wale ambao wamekuwa vipofu kwa sababu walilikataa Neno la Mungu. Hawa ndio wao waliovua nguo wakawa uchi kwa kuacha uangalizi na ulinzi wa Mungu wakatafuta kutengeneza njia yao wenyewe ya wokovu, mnara wao wenyewe wa Babeli kwa kuunda madhehebu.

Loo! jinsi wanavyoonekana wamevalia vizuri na malidadi mbele ya macho yao wenyewe wanapofanya mabaraza yao makubwa, na halmashauri zao, nk. Lakini sasa Mungu anayaweka yote wazi nao ni uchi, kwa maana madhehebu haya hayakufanya kitu ila yamewaongoza tu kwenye kambi ya mpinga-Kristo, kwenye mashamba ya magugu, moja kwa moja mpaka kwenye kufungwa matita-matita na kuteketezwa. Hao kweli ni vyombo vya kusikitikiwa. Naam, wasikitikieni, waonyeni, wabembelezeni, na hata hivyo wanaenda zao moja kwa moja kwenye uharibifu, wakipuuza kwa ghadhabu kali jitihada yo yote na jitihada zote za kuwaokoa kama vinga kutoka motoni wasiungue. Kweli hao ni wenye mashaka, hata hivyo hawajui. Wamekufa ganzi na hawana matumaini kabisa, wao wanajitukuza kwa jambo ambalo ni aibu yao kweli. Waliasio Neno, hata hivyo siku moja wao watahukumiwa kwalo na kulipa gharama ya mashtaka yake ya kutisha.

**USHAURI WA MWISHO WA NYAKATI**

Ufunuo 3:18-19.

> *"Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*
>
> *Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu."*

Shauri la Mungu ni fupi. Ni la maneno machache. Yeye analielekeza kanisa hili la wakati wa mwisho kwenye tumaini moja. Tumaini hilo ni YEYE MWENYEWE. Anasema, "Njoo Kwangu ukanunue." Ni dhahiri kutokana na fungu hili la maneno "ununue Kwangu" ya kwamba kanisa la Laodikia halishughuliki hata kidogo na Yesu kwa ajili ya matunda ya Kiroho ya Ufalme wa Mungu. Shughuli zao haziwezi kuwa ni za Kiroho. Wao wanaweza kufikiria kwamba ni wa Kiroho, lakini wanawezaje kuwa ni wa kiroho? Kazi wazitendazo kati yao kweli kabisa si kama vile ambavyo Paulo angesema, "Mungu atendaye kazi ndani yenu kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 2:13. Hivyo basi vipi kuhusu makanisa haya yote, shule, hospitali, juhudi za kimishenari, nk.? Mungu hayupo ndani ya hizo mradi tu wao ni uzao na roho wa kimadhehebu, na si wa Uzao na wa Roho wa Mungu.

*"Nunua Kwangu, dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri."*

Sasa watu hawa walikuwa na dhahabu nyingi sana, lakini ilikuwa ni ya aina isiyofaa. Ilikuwa ni ile dhahabu iliyoyanunua maisha ya wanadamu na kuwaangamiza. Ilikuwa ni ile dhahabu iliyopinga na kuipotoa tabia ya binadamu, kwa maana kuipenda kwake kulikuwa ndio chanzo cha maovu yote.

Ufunuo 18:1-14,

> *"Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.*
>
> *Akalia kwa nguvu kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu, umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;*
>
> *Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake.*
>
> *Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.*
>
> *Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.*
>
> *Mlipeni kama yeye alivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu.*
>
> *Kwa kadiri alivyojitukuza na kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo. Kwa kuwa husema moyoni mwake, Nimeketi malkia, wala si mjane, wala sitaona huzuni kamwe.*
>
> *Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu.*
>
> *Na hao wafalme wa nchi, waliozini naye na kufanya anasa pamoja naye, watalia na kumwombolezea; wauonapo moshi wa kuungua kwake;*
>
> *Wakisimama mbali kwa hofu ya maumivu yake, wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu, Babeli, mji ule ulio na nguvu! kwa kuwa katika saa moja hukumu yako imekuja.*

*Nao wafanya biashara wa nchi watalia na kumwombolezea, kwa sababu hapana mtu anunuaye bidhaa yao tena;*

*Bidhaa ya dhahabu, na fedha, na kito chenye thamani, na lulu, na kitani nzuri, na nguo ya rangi ya zambarau, na hariri, na nguo nyekundu; na kila mti wa uudi, na kila chombo cha pembe, na kila chombo cha mti wa thamani nyingi, na cha shaba, na cha chuma, na cha marimari;*

*Na mdalasini, na manukato, na iliki, na uvumba, na marhamu, na ubani, na mvinyo, na mafuta ya mzeituni, na unga mzuri, na ngano, na ng"ombe, na kondoo, na farasi, na magari, na watumwa na nafsi za wanadamu.*

*Na matunda yaliyotamaniwa na roho yako yamekuondokea; na vitu vyote vilivyo laini na vitu vya fahari vimekupotea; nawe hutaviona tena kamwe.*"

Haya ni kweli kabisa yale makanisa yaliyounda madhehebu ya siku za mwisho, kwa maana inasema katika aya ya 4, "Tokeni kwake ENYI WATU WANGU." Kunyakuliwa hakujatukia bado. Bibiarusi hajaondoka bado wakati hali hizi mbaya sana katika kanisa hili tajiri, la uongo zinapokuwepo.

Lakini, kuna dhahabu ya Mungu. I Petro 1:7.

*"Ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo."*

Dhahabu ya Mungu ni tabia iliyo kama ya Kristo iliyotengenezwa katika tanuru ya moto wa mateso. Hiyo ndiyo dhahabu inayofaa.

Lakini kanisa lina dhahabu ya namna gani leo? Halina kitu ila dhahabu ya dunia ambayo itaangamia. Ni tajiri. Linajikinai. Limefanya utajiri kuwa ndio kipimo halisi cha kuwa wa kiroho. Ushuhuda wa baraka za Mungu na usahihi wa mafundisho, nk. unategemea sasa ni matajiri wangapi wanahusika katika hayo.

"Afadhali uje kabla hujachelewa," asema Bwana, "na ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ndipo utakuwa tajiri kweli." Je! Tunalipata? Nisikilizeni mimi, "Tunakuja uchi (kimwili) ulimwenguni, lakini HATUTAUACHA (kiroho) tukiwa uchi." Loo la, tutabeba kitu fulani. Kwamba kitu hicho ni nini, ndicho TU tunachoweza kubeba, si pungufu wala si zaidi. Kwa hiyo afadhali tuwe waangalifu sana sasa kuona ya kwamba tunachukua kitu kitakachotufanya sawa mbele za Mungu. Kwa hiyo, basi, tutabeba nini? Tutabeba TABIA yetu, ndugu, hiyo ndiyo tutakayochukua? Sasa utachukua tabia ya namna gani? Je! itakuwa kama Yake Yeye ambaye tabia yake ilifinyangwa kwa kuteseka katika tanuru ya moto ya mateso, ama itakuwa huu wororo wa watu hawa wa Laodikia wasio na tabia njema? Ni juu yetu kila mmoja wetu, kwa kuwa katika siku hiyo kila mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe.

Sasa, nilisema ya kwamba mji wa Laodikia ulikuwa ni mji tajiri. Ulitengeneza sarafu za dhahabu zilizoandikwa pande zote. Sarafu za dhahabu ziliainisha wakati huo—kulikuwako na biashara iliyostawi kwa ajili ya hizo. Leo, ile sarafu ya dhahabu yenye pande mbili iko pamoja nasi. Tunajilipia kutoka na tunajilipia kuingia. Kanisani, tunajaribu kufanikisha jambo lile lile. Tunajilipia kutoka dhambini na kujilipia kuingia mbinguni—ama ndivyo tusemavyo. Lakini Mungu hasemi jambo hilo.

Kanisa linamiliki utajiri usio wa kawaida, hivi kwamba katika wakati wo wote ule linaweza kutwaa madaraka yote ya mpango wa biashara ya dunia, na kwa kweli kiongozi fulani wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni ametabiri hadharani ya kwamba kanisa katika siku zijazo litapaswa, litaweza, na litafanya hasa jambo hilo. Lakini mnara wao wa dhahabu wa Babeli utaanguka. Dhahabu iliyojaribiwa katika moto tu ndiyo itakayostahimili.

Na hivyo ndivyo ambavyo kanisa limefanya daima katika zile nyakati. Limeliacha Neno la Mungu na kuchukua kanuni zake lenyewe za imani na mafundisho ya sharti; limejifanya madhehebu na kujiunganisha lenyewe na ulimwengu. Hivyo basi liko uchi, na Mungu anahukumu uasherati wake. Njia pekee linaloweza kutoka kwenye hali hii mbaya sana ni kwa kumtii Bwana kurudi kwenye Neno Lake.

Ufunuo 18:4,

*"Tokeni Kwake enyi watu Wangu."*

II Wakorintho 6:14-18.

*"Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza?*

*Tena pana mapatano gani kati ya Kristo na Beliari? au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini?*

*Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? kwa maana ninyi ni*

*hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.*

*Kwa hiyo, Tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.*

*Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi."*

Kuna malipo ya kulipa kwa ajili ya mavazi hayo, na hayo ni malipo ya kutengana.

*"Na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."*

Yeye hasemi ya kwamba inakubidi kununua dawa hii ya macho. Loo, la. Roho Mtakatifu hauzwi.

*"Je! mlimpokea Roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani?"*

Wagalatia 3:2.

Bila Ubatizo wa Roho Mtakatifu, macho yako hayawezi kufunguliwa upate ufunuo wa kweli wa Kiroho wa Neno. Mtu asiye na Roho ni kipofu kwa Mungu na kweli Yake.

Ninapofikiria juu ya dawa hii ya macho kuyafungua macho ya watu, karibu siwezi kujizuia kukumbuka wakati nilipokuwa mvulana mdogo huko Kentucky. Mimi pamoja na ndugu yangu tulilala katika orofa ndogo ya juu kabisa kwenye godoro la manyasi. Mianya ya nyufa za nyumba hiyo ingeingiza baridi. Wakati mwingine katika majira ya kipupwe kungekuwa na baridi sana kwamba tungeamka asubuni macho yetu yakiwa yamefumbwa kabisa yakagandamana kwa baridi hata yakavimba na kuuma. Tungemlilia mama, naye angekuja akiwa na mafuta yenye moto ya mnyama aina ya cheche na kuyasugua macho yetu mpaka usaha uliokauka ungetoka, na ndipo tungeweza kuona.

Unajua kumekuwako na baridi mbaya sana inayovuma katika kanisa katika kizazi hiki, nami nachelea macho yake kwa namna fulani yamegandamana yakafunga kwa baridi nalo ni kipofu kwa yale Mungu aliyo nayo kwa ajili yake. Linahitaji mafuta ya moto ya Roho wa Mungu kuyafungua macho yake. Lisipompokea Roho wa Mungu litaendelea kubadilisha nguvu kwa utaratibu na Neno kwa kanuni za imani. Linahesabu idadi kwamba ndiyo mafanikio, badala ya kutafuta matunda. Madaktari wa theolojia wameufunga mlango wa imani na kuwakataza wote kuingia. Wao wenyewe hawaingii, wala hawaruhusu mtu mwingine aingie. Theolojia yao inatoka kwenye kitabu cha saikolojia kilichoandikwa na mtu fulani asiyeamini. Kuna kitabu cha maandishi juu ya saikolojia, kimoja tunachohitaji sisi sote; ni Biblia. Kimeandikwa na Mungu na kina saikolojia ya Mungu. Huhitaji daktari ye yote kukielezea kwako. Mpokeeni Roho Mtakatifu na mwacheni akielezee. Yeye aliandika kile Kitabu na Yeye anaweza kukwambia kilichomo ndani yake na maana yake.

I Wakorintho 2:9-16

*"Lakini kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.*

*Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho, maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.*

*Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.*

*Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.*

*Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho Mtakatifu, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*

*Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni. Lakini mtu wa Rohoni huyatambua yote, wala yeye mwenyewe hatambuliwi na mtu.*

*Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, kwamba amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo."*

Sasa kama mambo yote ambayo Roho analia dhidi yake ni kweli kwa wakati huu, tunahitaji mtu fulani ajitokeze kama alivyofanya Yohana Mbatizaji na kulipinga kanisa kuliko ilivyokuwa hapo awali. Na hilo ndilo hasa linalokuja kwenye wakati wetu. Yohana Mbatizaji mwingine anakuja naye atapiga makelele hasa kama alivyofanya mtangulizi wa kwanza. Tunajua ya kwamba atafanya hivyo kwa sababu ya aya inayofuata.

*"Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu."*

Ufunuo 3:19.

Huu ndio ujumbe ule ule aliokuwa nao Yohana alipokuwa akipiga kelele katika lile jangwa la kidini la Mafarisayo, Masadukayo, na makafiri, "TUBUNI!" Hapakuwepo na njia nyingine wakati huo; hakuna nyingine sasa. Hakukuwa na njia nyingine ya kumrudia Mungu wakati huo, na hakuna njia nyingine sasa. Ni TUBUNI. Badili nia yako. Geukeni. TUBUNI, kwa maana kwa nini mfe?

Hebu na tuchunguze fungu la kwanza la maneno, "wote niwapendao." Katika Kiyunani mkazo upo kwenye kijina cha nafsi "MIMI". Hasemi wengi ambao wangejisikia angesema, "wote wanipendao MIMI." La bwana. Hatupaswi kamwe kujaribu kumfanya Yesu kuwa KITU cha kupendwa na mwanadamu katika aya hii. La! Ni WOTE walio WAPENDWA wa Mungu. Upendo WAKE, ndio tunaozungumzia, SI wetu.

Kwa hiyo mara nyingine tena tunajikuta tukifurahia katika wokovu Wake, kusudi Lake na mpango Wake, nasi tunaimarika hata na zaidi katika kweli ya fundisho la Ukuu wa Mungu. Kama tu vile alivyosema katika Rum. 9:13. "Nimempenda Yakobo." Je! sasa ina maana ya kwamba kwa kuwa Yeye aliwapenda hao WENGI TU, Yeye sasa yuko katika hali ya kinaya, akingojea upendo wa hao ambao hawajamkaribia? Hivi sivyo lilivyo kabisa, kwa maana Yeye alitangaza pia katika Rum. 9:13, "Esau nimemchukia." Na katika aya ya 11 Roho anasema kwa ujasiri, "Kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ILI LISIMAME KUSUDI LA MUNGU LA KUCHAGUA, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia Yake aitaye." Upendo huu ni "Upendo wa kuchagua". Ni upendo Wake kwa wateule Wake. Na upendo Wake kwao hauhusiki na KUSTAHILI KWA KIBINADAMU kwa maana inasemwa ya kwamba kusudi la Mungu linasimama katika kuchagua jambo ambalo ni kinyume kabisa cha kazi wala cho chote alicho nacho binadamu mwenyewe. Kwa kuwa "KABLA HAWAJAZALIWA WALE WATOTO" Yeye TAYARI alikuwa amekwisha kusema, "Nimempenda Yakobo, lakini Esau nimemchukia."

Na sasa anawaambia walio Wake, "Wote niwapendao Mimi, NAWAKEMEA NA KUWARUDI." Kukemea ni kukaripia. Kukaripia ni „kuweka wazi kwa ajili ya kusahihisha." Kurudi hakumaanishi kuadhibu. Kunamaanisha kumkanya mtu kwa sababu nia ni kumsahihisha."

Hili ndilo hasa tunalopata katika Waebrania 12:5-11,

> *"Tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana, Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa Naye;*
>
> *Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye.*
>
> *Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye?*
>
> *Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali.*
>
> *Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi?*
>
> *Maana ni hakika, hao kwa siku chache walituruđi kama walivyoona vema wenyewe; bali Yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu Wake.*
>
> *Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani."*

Hapa basi unaonyeshwa upendo wa Mungu. Yeye alitamani jamaa Yake Mwenyewe katika upendo, jamaa ya wana—wana kama Yeye. Hapo mbele Yake wamekaa wanadamu wote kama bonge MOJA la udongo. Kutoka kwenye lundo lilo hilo sasa atafanya vyombo vya heshima na visivyo vya heshima. UCHAGUZI Utakuwa ni kuchagua Kwake mwenyewe. Ndipo hao aliowachagua, waliozaliwa kwa Roho Wake Watafundishwa kufanana na sura Yake katika mwenendo wao. Yeye HUKARIPIA kwa uvumilivu wote na upole na rehema. Yeye HURUDI kwa mikono yenye makovu ya misumari. Wakati mwingine Mfinyanzi huyu hana budi kuchukua chombo anachokifanyia kazi na kukivunja-vunja kabisa kabisa kusudi apate kukiunda tena jinsi anavyokitaka hasa. LAKINI NI UPENDO. HUO NI UPENDO WAKE. HAKUNA NJIA NYINGINE YA UPENDO WAKE. HAIWEZI KUWAKO.

Loo, enyi kundi dogo, msiogope. Wakati huu unamalizika upesi. Na unapomalizika magugu hayo yatafungwa pamoja, na kama vile kamba ya nyuzi tatu haikatiki upesi, yatakuwa yenye nguvu nyingi sana za namna tatu za kisiasa, kimwili, na kiroho (Kishetani), nayo yatatafuta kumwangamiza bibi-arusi wa Kristo. Atateseka, bali atavumilia. Usiogope mambo hayo yanayokuja juu ya dunia, kwa maana Yeye "Ambaye aliwapenda watu Wake, aliwapenda upeo." Yohana 13:1.

*"Uwe na bidii ukatubu."* Sasa kanisa hili la uongo lina bidii; usikosee juu ya jambo hilo. Bidii yake kweli

imekuwa ile ya Wayahudi,

Yohana 2:17,

*"Wivu wa nyumba yako umenila."*

Lakini ni bidii mbaya. Ni ya nyumba waliyojijengea wenyewe. Ni ya kanuni zao wenyewe, mafundisho ya sharti, madhehebu, haki yao wenyewe. Wameliondosha Neno wakatwaa mawazo yao wenyewe. Walimwondoa Roho Mtakatifu na kuwafanya wanadamu kuwa viongozi. Wameweka kando Uzima wa Milele kama Mtu, na kuufanya kwamba ni matendo mema, ama hata kuigiza kanisa badala ya matendo mema.

Lakini Mungu anahitaji bidii nyingine. Ni bidii ya kulia "NIMEKOSA". Sasa ni nani atakayesema ya kwamba amekosea? Ni kitu gani madhehebu haya yote yanachotegemea?—dai la uanzilishi, pia dai la Mungu,—dai la kwamba wao ndio walio wa kweli. Sasa WOTE hawawezi kuwa sahihi. Kwa kweli HAKUNA MMOJA wao aliye sahihi. Ni makaburi yaliyopakwa chokaa, yamejaa mifupa ya watu waliokufa. Hayana uhai. Hayana thibitisho. Mungu hajajijulisha kamwe katika madhehebu yo yote. Wao wanasema wako sahihi kwa sababu wao ndio wanaosema jambo hilo, lakini kusema kitu hakukifanyi kuwa kweli. Wao wanahitaji "Bwana asema hivi" iliyothibitishwa ya Mungu, nao hawanayo.

Sasa hebu niseme jambo hili hapa. Siamini ya kwamba Mungu anaita kanisa la uongo peke yake kuja kutubu. Katika aya hii Yeye anazungumza na wateule Wake. Wao wana jambo la kutubia, pia. Wengi wa watoto Wake wangali wako kwenye hayo makanisa ya uongo. Hao ni wale ambao habari zao zinasemwa katika Efe. 5:14, *"Amka, wewe usinziaye, ufufuke katika wafu, na Kristo atakuangaza."* Kulala si kufa. Hawa wamelala miongoni mwa wafu. Wako huko nje katika madhehebu yaliyokufa. Wanaelea pamoja nao. Mungu anapaza sauti, "AMKENI! Tubieni ujinga wenu." Hawa hapa wakitoa ushawishi wao, wakitoa wakati wao na fedha zao, kwa kweli maisha yao yenyewe kwa haya madhehebu ya mpinga-Kristo, na wakati wote wakifikiria kila kitu ni kweli. Wanahitaji kutubu. Hawana budi kutubu. Wanahitaji kuwa na badiliko la nia na kugeukia kweli.

Naam, huu ndio wakati ambao wengi wanahitaji kutubu. Lakini utatubu? Utalirudisha Neno? Je! utamrudisha tena Roho Mtakatifu kwenye kiti cha enzi katika maisha ya watu? Utamheshimu tena Yesu kama Mwokozi PEKEE? Ninasema la, kwa maana aya inayofuata inaonyesha ukweli wa kushangaza sana na wa kufadhaisha sana wa kumalizia kwa wakati huu.

**KRISTO AKIWA NJE YA KANISA**

Ufunuo 3:20- 22,

*"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.*

*Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Sasa kuna utata mkubwa sana juu ya aya hii kwa sababu wengi sana wanaotenda kazi kibinafsi katika uinjilisti wa kibinafsi wanautumia kana kwamba Yesu alikuwa kwenye mlango wa moyo wa kila mwenye dhambi akipiga hodi apate kuruhusiwa kuingia. Ingesemwa basi ya kwamba kama mwenye dhambi angefungua mlango, Bwana angeingia. Lakini aya hii haizungumzi na wenye dhambi binafsi. Ujumbe huu wote una muhtasari kama ilivyo kila ujumbe katika kila wakati. Katika aya ya 22 inasema, *"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia MAKANISA."* Kwa hiyo huu ndio ujumbe kwa kanisa la wakati wa mwisho. Hii ndiyo hali ya kanisa la Laodikia wakati mwisho wake unapokaribia. Si ujumbe wa kibinafsi kwa mtu mmoja; ni Roho akituambia mahali Yesu alipo. KRISTO AMELIACHA KANISA.

Je! hayo siyo matokeo dhahiri ama mwisho kama Neno likiwekwa kando badala ya kanuni ya imani kuweka kando, Roho Mtakatifu akiondolewa na mapapa, maaskofu, marais, washauri, nk. kuchukua mahali Pake, na Mwokozi akiwekwa kando na badala Yake nafasi ichukuliwe na utaratibu wa shughuli za kidini, ama kujiunga na kanisa, ama namna fulani ya kupatana na utaratibu wa kanisa? Kuna nini zaidi linaloweza kufanywa dhidi Yake? Huu ni ukengeufu! Huku ni kuanguka! Huu ni mlango uliofunguliwa kwa mpinga-Kristo, kwa maana kama Mmoja alikuja katika Jina la Baba Yake (Yesu) wala hakupokewa, lakini akakataliwa, basi atakuja mwingine aliye na jina lake mwenyewe (mwongo, mnafiki) naye huyo wao watampokea, Yohana 5:43. Mtu wa dhambi, huyo mwana wa upotevu atachukua mamlaka.

Mt. 24, inataja ishara mbinguni kuhusu siku hii ya mwisho kabla tu ya kuja kwa Yesu. Sijui kama uliona ishara kama hiyo hivi majuzi ikitimizwa ipate kuonyesha kweli ile ile tuliyokuwa tukinena habari zake. Kweli hiyo ni kwamba Yesu amekuwa akisukumwa pole pole kando mpaka katika wakati wa mwisho amesukumwa nje ya kanisa. Kumbuka ya kwamba katika wakati wa kwanza kanisa lilikuwa karibu ni mviringo mzima wa kweli. Walakini kulikuweko na kosa dogo lililoitwa matendo ya wanikolai lililoifanya

duara hiyo kutojaa. Ndipo katika wakati uliofuata giza zaidi lilipenya mpaka ile duara ya nuru ikapunguza mwangaza wake, ndipo giza likafunika sehemu kubwa zaidi ya ile duara. Katika wakati wa tatu ilifunikwa hata na zaidi, na katika wakati wa nne ambao ulikuwa ndio zile Zama za Giza, nuru ilikuwa karibu yote imekwisha.

Sasa fikiria juu ya jambo hili. Kanisa linaangaza katika nuru iliyotoka kwa Kristo. Yeye ndiye JUA. Kanisa ni MWEZI. Kwa hiyo mviringo huu wa nuru ni mwezi. Ulikuwa umepungua kutoka karibu mwezi mzima katika wakati wa kwanza, kufikia kipande chembamba katika wakati wa nne. Lakini katika wakati wa tano ulianza kukua. Katika wakati wa sita ukapiga hatua kubwa sana ya kukua kuendelea mbele. Katika sehemu ya wakati wa saba ulikuwa ungali unakua, ndipo mara moja ukakoma, na ukafifia karibu kabisa, hivi kwamba badala ya nuru ilikuwa ni giza la ukengeufu, na katika mwisho wa wakati ulikuwa umeacha kuangaza kwa maana giza lilikuwa limeshinda. Kristo sasa alikuwa nje ya kanisa.

Hii hapa ile ishara mbinguni. Kule kupatwa kwa mwisho kwa mwezi kulikuwa kupatwa kwa mwezi wote. Ulififia ukawa giza tupu katika hatua saba. Katika hatua ya saba, giza tupu liliingia wakati Papa wa Roma (Paulo wa Sita) alipoenda huko Palestina kufanya ziara takatifu ya Yerusalemu. Alikuwa ndiye papa wa kwanza aliyepata kwenda Yerusalemu. Huyo papa anaitwa Paulo wa Sita. Paulo alikuwa ni mjumbe wa kwanza na mtu huyu anaitwa kwa jina hilo. Angalia kwamba ni wa sita, ama hesabu ya mwanadamu. Hii ni zaidi ya kubahatisha. Na hapo alipokwenda Yerusalemu, mwezi ama kanisa likawa giza tupu. Mambo ndiyo hayo. Huu ndio ule mwisho. Kizazi hiki hakitapita mpaka yote yatakapotimizwa. Naam Bwana Yesu, njoo upesi!

Sasa tunaweza kuona ni kwa nini kulikuweko na mizabibu miwili, mmoja wa kweli na mmoja wa uongo. Sasa tunaweza kuona ni kwa nini Ibrahimu alikuwa na wana wawili, mmoja wa kimwili (aliyemtesa Isaka) na mmoja wa ahadi. Sasa tunaweza kuona ni kwa nini kwamba kutoka kwa wazazi wale wale wavulana wawili walitokea kama mapacha, mmoja akipenda na kuyajua mambo ya Mungu, na yule mwingine akijua mengi ya kweli hiyo hiyo, lakini hakuwa wa Roho yule yule, na kwa hiyo akamtesa mtoto aliyekuwa ameteuliwa. Mungu hakukataa vivi hivi tu kwa ajili tu ya kukataa. Yeye alikataa kwa ajili ya wateule. MTEULE HAWEZI kumtesa mteule. MTEULE HAWEZI kumdhuru mteule. Waliokataliwa ndio wanaowatesa na kuwaangamiza wateule. Loo, hao waliokataliwa ni wa kidini. Wao ni werevu. Wao ni wa ukoo wa Kaini, uzao wa nyoka. Wanajenga Babeli zao, wanajenga miji yao, wanajenga milki zao, na wakati wote wanamwita Mungu. Wanachukia uzao wa kweli, nao watafanya yote wawezayo, (hata katika Jina la Bwana) kuwaangamiza wateule wa Mungu. Lakini wanahitajika. "Makapi yana faida gani kwa ngano?" Bila makapi, hakuna ngano. Lakini mwishoni, inakuwaje kwa makapi? Yanateketezwa kwa moto usiozimika. Na hiyo ngano? Iko wapi? Imekusanywa katika ghala Lake. Ni mahali Yeye alipo.

Enyi wateule wa Mungu, jihadharini. Chunguzeni kwa makini. Kuweni waangalifu. Utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka. Mtegemeeni Mungu na mwe hodari katika uweza Wake. Adui yenu, ibilisi, hata sasa anazunguka-zunguka kama simba angurumaye akitafuta mtu ammeze. Kesheni katika maombi na mwe imara. Huu ni wakati wa mwisho. Mizabibu yote miwili wa kweli na wa uongo inafikia kukomaa, lakini kabla ngano haijakomaa, magugu hayo yaliyoiva hayana budi kufungwa yapate kuteketezwa. Mnaona, yote yanajiunga na Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Huko ndiko kule kufungwa. Hivi karibuni utafika wakati wa ngano kuwekwa ghalani. Bali sasa hivi zile roho mbili zinatenda kazi katika ile mizabibu miwili. Tokeni kati ya hayo magugu. Anzeni kushinda mpate kuhesabiwa wanaostahili sifa kwa ajili ya Bwana wenu, na wanaostahili kumiliki na kutawala pamoja Naye.

**KITI CHA ENZI CHA MWENYE KUSHINDA**

Ufunuo 3:21,

> *"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi."*

Sasa tunapaswa kushinda nini? Hilo ndilo swali la kawaida la kuuliza hapa. Lakini hilo silo wazo halisi la aya hii kwa maana sana sana si YALE tunayopaswa kushinda bali ni JINSI tunavyopaswa kushinda. Sasa hili ni wazi, kwa maana je! ni hoja sana YALE tunayopaswa kushinda iwapo tunajua JINSI ya kushinda?

Mtazamo wa haraka wa yale Maandiko yanayomhusu Bwana Yesu akishinda yataelezea ukweli wa hoja hii. Katika Mt. 4, ambapo Yesu anajaribiwa na ibilisi, Yeye alishinda hayo majaribu ya binafsi ya Shetani kwa Neno, na kwa Neno peke yake. Katika kila moja ya yale majaribu matatu makuu yaliyofanana kabisa na yale majaribu ya Bustani ya Edeni, tamaa ya mwili, tamaa ya jicho, na kiburi cha uzima, Yesu alishinda kwa Neno. Hawa alianguka kwa jaribu la kibinafsi la Shetani kwa kushindwa kutumia Neno. Adamu alianguka kwa kutolitii Neno waziwazi. Lakini Yesu alishinda kwa Neno. Lakini Yesu alishinda kwa Neno. Na sasa hivi, hebu niseme ya kwamba hii ndiyo njia pekee ya kuwa mshindi, pia ndiyo njia pekee ambayo unaweza kujua kama unashinda, kwa maana hilo Neno HALIWEZI kushindwa.

Sasa angalia tena jinsi Yesu alivyoshinda utaratibu wa dini za ulimwengu. Wakati aliposumbuliwa mara

kwa mara na wanatheolojia wa siku Yake, Yeye daima alitumia Neno. Yeye alinena tu yale Baba aliyompa kunena. Hapakuwepo na wakati ambapo ulimwengu haukuwa umetatanishwa kabisa na hekima Yake kwa maana ilikuwa ni hekima ya Mungu.

Katika maisha Yake ya kibinafsi, akishindana na nafsi Yake, Yeye alishinda kwa kulitii Neno la Mungu.

Katika Waebrania 5:7 inasema,

> *"Yeye, siku hizo za mwili Wake, alipomtolea yule awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu;*
>
> *Ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata;*
>
> *Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."*

Yeye alikuwa mtii kwa kitu gani? Neno la Mungu.

Sasa basi, hakutakuwako na mtu hata mmoja atakayeketi katika kiti cha enzi cha Bwana Yesu Kristo isipokuwa amekuwa akiliishi hilo Neno. Maombi yenu, kufunga kwenu, toba zenu—haidhuru umpe nini Mungu—hakuna hata moja ya hayo yatakayokupa majaliwa ya kuketi kwenye kiti hicho cha enzi. Bibi-arusi NENO tu ndiye atakayejaliwa. Kama vile kiti cha enzi cha mfalme hushirikishwa malkia kwa sababu ameungana naye, vivyo hivyo ni wale tu walio wa Neno kama vile Yeye alivyo wa hilo Neno watashiriki kiti hicho cha enzi.

Kumbukeni tumeonyesha wazi wazi katika nyakati zote ya kwamba kama vile Adamu na Hawa walivyoanguka kwa sababu waliliacha Neno, vivyo hivyo Wakati wa Efeso ulianguka kwa kugeuka kidogo kutoka kwenye Neno, mpaka na kila wakati ukiendelea kugeuka, tumefikia kukataliwa kwa mwisho kwa Neno na utaratibu wa Kanisa la Ulimwengu. Wakati huu wa Laodikia unaishia katika kutiwa giza kabisa kwa Neno, na kwa hiyo kumfanya Bwana kuondoka katikati yao. Anasimama nje akiita walio Wake wanaomfuata Yeye kwa kulitii Neno. Baada ya dhihirisho fupi na lenye nguvu la Roho kundi hili dogo linalowindwa na kuteswa litaondoka liende kuwa pamoja na Yesu.

**MWISHO WA NYAKATI ZA MATAIFA**

Wakati huu ndio wa mwisho wa zile nyakati saba za kanisa. Kile kilichoanza katika Wakati wa Kwanza au Wakati wa Efeso hakina budi na lazima kifikie kwenye ukamilifu wa kutoa mazao na kuvunwa katika ule wa mwisho ama Wakati wa Laodikia. Hiyo mizabibu miwili itazaa matunda yake ya mwisho. Roho hizo mbili zitamaliza dhihirisho lao katika kila moja ya vikomo vyao vya mwisho. Kule kupanda, kule kumwagia maji, kule kukua kote kumekwisha. Majira ya kiangazi yamekwisha. Mundu sasa umetupwa katika mavuno.

Katika aya ya 15 mpaka ya 18 ambazo ndiyo tu tuzisome kuna picha ya kweli ya mzabibu wa uongo ulioiva, roho wa uongo, watu wa kanisa la uongo. *"Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; Ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakupa shauri, ununue Kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri; na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona."* Hakuna maneno yaliyopata kuonyesha kukataliwa kuchungu zaidi, wala hakuna watu wa kidini wenye kiburi na wanaojivuna waliostahili hayo zaidi ya hao.

Hata hivyo katika aya ya 21,

> *"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi,"*

Tunaona ule mzabibu wa kweli, Roho wa kweli, watu wa Kanisa la kweli wameinuliwa mpaka kwenye kiti cha enzi cha Mungu na sifa za hali ya juu sana zilizopata kutolewa kwa kundi imara la Kiroho na nyenyekevu.

Maneno ya Yohana Mbatizaji aliyemweleza Kristo kwa usahihi sana katika uhusiano wa kanisa la kweli na la uongo sasa yanatimia.

Mathayo 3:11-12,

> *"Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali Yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko Mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu Vyake; Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.*
>
> *Ambaye pepeto Lake li mkononi Mwake, Naye atausafisha uwanda Wake; na kuikusanya*

*ngano Yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika."*

Kristo, yule Mvunaji Mkuu, sasa anavuna matunda ya nchi. Yeye anaikusanya ngano ghalani kwa kuja kwa ajili ya walio Wake na kuwapokea milele Kwake. Ndipo anarudi kuwaangamiza waovu kwa moto usiozimika.

Ile siri ya magugu na ngano ya Mt. 13:24-30, hivi sasa pia imetimizwa.

*"Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake:*

*Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.*

*Baadaye majani ya ngano yalipomea, na kuzaa, yakaonekana na magugu.*

*Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu?*

*Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye?*

*Lakini akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing"oa ngano pamoja nayo.*

*Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani Mwangu."*

Ngano na magugu, ambavyo tangu wakati ule wa kwanza hata sasa vimekua pamoja, vinavunwa. Yale ambayo Nikea ilitaka kutimiza hatimaye yametimwizwa sasa. Likiwa na nguvu zote za madhehebu kanisa la uongo linaacha kila kweli dalili yote ya kweli na kwa nguvu za kisiasa linajiimarisha huku likisaidiw na serikali na linatoka kwenda kumwangamiza kabisa mwamini wa kweli. Lakini wakati tu ambapo liko karibu na kutimiza njama zake za woga ngano inakusanywa ghalani. Ngano na magugu hayatamea pamoja tena. Magugu hayatapokea baraka za Mungu tena kwa sababu ya uwepo wa ngano, kwa maana ngano itakuwa imeondoka na ghadhabu ya Mungu itamwagwa katika muhuri ya sita ambao utaishia katika maangamizi kabisa ya walio waovu.

Sasa nilisema muda mfupi uliopita ya kwamba ule mzabibu wa uongo ulikomaa kikamilifu katika wakati huu. Tunda lake lingepevuka na kukomaa. Hilo ni kweli. Kanisa hili lililo na roho mchafu, lililojaa uovu, litafunuliwa kama mbegu ya haradali iliyokua ikawa mti ambamo mlikaa ndege wa angani. Kiongozi wake atakuwa mpinga-Kristo, ile siri ya kuasi. Yote haya ni kweli. Na kama hii ni kweli, basi haina budi kuwa ni kweli ya kwamba kanisa la Bibi-arusi litakomaa, na kuiva kwake kutakuwa ni kujitambulisha na Bwana wake kwa njia ya Neno, na Kiongozi Wake Ambaye atakuja kwake ni ile Siri ya Uungu, Ambayo kweli ni Kristo. Na kama vile kanisa la uongo likiwa na ujanja wote na nguvu za ibilisi zilizoundwa kwa nguvu za kisiasa, nguvu za kimwili na mapepo ya giza litakapokuja kupiga vita mzabibu huu wa kweli, ule mzabibu wa kweli ukiwa na utimilifu wa Roho na Neno utafanya matendo yale yale ya nguvu ambayo Yesu alifanya. Ndipo wakati linapokaribia jiwe lake la Kileleni, likifanyika kama Yeye kupitia katika Neno, Yesu atakuja kusudi bibi-arusi na Bwana-arusi waunganike kama mmoja milele.

Tayari madhihirisho yanayoonekana ya yale nilivyokuwa nikiwaambia yanaonekana kila upande. Pilikapilika za ekumeni za magugu ni jambo la kweli. Lakini pia ni kweli ya kwamba nabii wa wakati wa mwisho hana budi kuwa analeta ujumbe kutoka kwa Mungu ambao utakutangulia kuja kwa Bwana mara ya pili, kwa kuwa kwa ujumbe wake ndipo mioyo ya watoto itawarudia baba zao wa Pentekoste, na pamoja na kurudishwa kwa Neno kutakuja kurudishwa kwa zile nguvu.

Ni nyakati za uamuzi mzito zilizoje hizi tunazoishi. Jinsi tunavyopaswa kuwa waangalifu kusudi tudumu waaminifu kwa Neno hili wala tusiondoe kwake wala kuongeza kwake, kwa maana yeye ambaye angenena ambapo Mungu hajanena anamfanya Yeye mwongo. Jambo nililo nalo moyoni hasa ni hili: Kufikia mwisho wa karne hii njaa ya Mungu iliyoanzia kwenye Wakati wa Filadelfia ilisababisha kulilia Roho wa Mungu. Na wakati kilio hicho kilipojibiwa na Mungu kwa kutuma madhihirisho katika lugha, kufasiri na unabii, mara kundi fulani, na likiwa kinyume kabisa cha Neno, lilianzisha fundisho ya kwamba lugha zilikuwa ndizo ushuhuda wa kubatizwa na Roho Mtakatifu. Lugha zilikuwa mbali na ushuhuda. Zilikuwa dhihirisho, lakini si ushahidi. Uongo wa fundisho hilo hauwezi kuonekana tu kwa ukosefu wa Maandiko kuyakinisha jambo hilo, lakini hao waliofuata fundisho hilo waliunda madhehebu mara moja juu ya msingi wa fundisho hilo, ikithibitisha ya kwamba wao hawakuwa katika ile kweli kama walivyowataka watu waamini. Loo! lilionekana kwamba ni zuri. Lilionekana kama ni kule kurudi kwa Pentekoste. Lakini ilithibitika kwamba haikuwa hivyo. Haingeweza kuwa, kwa maana waliunda madhehebu. Hiyo ni mauti, si uzima. Ilionekana inafanana sana na kile kitu halisi hata wengi walidanganywa.

Sasa kama haikuwa ni kile kitu halisi, ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni ganda, kapi. Katika kifuniko kama ala ya kijani kibichi ilionekana kana kwamba ilikuwa ni kile kitu chenyewe. Lakini kama vile mtu anavyoweza kwenda shambani na kuona kile kinachoonekana kama ngano kabisa na walakini ni ganda tu, (kwa kuwa chembe ya ngano haijaumbika bado) kwa hiyo hili lilikuwa tu ni lile ganda laini ambalo lilionekana kama ile chembe halisi itakayokuja Ile chembe halisi ya Pentekoste ilikuwa irudi katika wakati wa mwisho. Ilikuwa imezikwa hapo Nikea. Ilitoa chipukizi wakati wa Sardi. Ikazaa kishada wakati wa Filadelfia, na ilikuwa ikomae wakati wa Laodikia. Lakini haingeweza kurudia ile ya asili mpaka Neno liliporudishwa. Nabii hakuwa amejitokeza katika sehemu ya tukio. Lakini sasa kulingana na wakati tunaposimamia katika Wakati wa Laodikia, „Nabii-Mjumbe" wa Ufu. 10:7 hana budi kuwa nchini tayari. Mara nyingine tena "Bwana asema hivi" haina budi kuwa hapa, tayari kudhihirishwa kwa ushuhuda usiokosea. Hivyo basi ile Mbegu ya Kweli tayari inakomaa, na HALAFU MAVUNO.

Wakati wa mavuno. Naam, wakati wa mavuno. Ile mizabibu miwili iliyokua pamoja na kukingamanisha matawi yake sasa haina budi kutenganishwa. Matunda ya mizabibu hiyo ambayo ilikuwa ikitofautiana yatakusanywa katika maghala tofauti. Roho hizo mbili zitakwenda kwenye vikomo vyao tofauti. Sasa ni wakati wa kuitikia ule mwito wa mwisho unaokuja tu kwa Bibi-arusi Ngano, „Tokeni kwake enyi watu Wangu msije mkashiriki dhambi zake, na ili kwamba ninyi (ngano) msipokee mapigo (ile dhiki kuu ya ile muhuri ya sita na Mt. 24) yake (magugu).

**ONYO LA MWISHO LA ROHO**

Ufunuo 3:22,

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Hili ndilo onyo la Mwisho. Hakutakuwako na lingine. Kile chumba chenye kiti cha enzi kimeandaliwa. Misingi hiyo kumi na miwili imewekwa. Barabara za dhahabu zimetengenezwa. Malango ya lulu makubwa mno yamesimamishwa na kufungwa bawabu. Hicho chumba kinasimama kama piramidi kikiwa malidadi sana na kizuri. Vile viumbe vya mbinguni vilivyokiandaa vinakiangalia kwa mshangao mkubwa mno, kwa maana kinametameta na kuangaza kwa utukufu usio wa duniani. Kila sehemu ya uzuri wake inasimulia hadithi ya neema ya ajabu na upendo wa Yesu. Ni mji uliotayarishwa kwa ajili ya watu waliofanywa tayari. Unangojea tu wenyeji wake na mara watajaa kwenye barabara zake kwa furaha. Naam, ni mwito wa mwisho. Roho hatanena katika wakati mwingine. Zile nyakati zimekwisha.

Lakini Mungu ashukuriwe, wakati huu, wakati huu haujakwisha. Yeye angali analia. Na kilio Chake hakiko tu katika masikio ya kiroho ya wanadamu kwa njia ya Roho Wake, lakini kwa mara nyingine tena nabii yuko nchini. Mara nyingine tena Mungu atafunua kweli kama alivyomfunulia Paulo. Katika siku za mjumbe wa saba, katika siku za Wakati wa Laodikia, mjumbe wake atafunua siri za Mungu kama zilivyofunuliwa kwa Paulo. Yeye atanena, na hao watakaompokea nabii huyo katika jina lake mwenyewe watapokea matokeo mema ya huduma ya nabii huyo. Nao hao watakaomsikia watabarikiwa na kuwa sehemu ya yule bibi-arusi wa siku ya mwisho ambaye anatajwa katika Ufunuo 22:17,

*"Roho na bibi-arusi wanasema njoo."*

Ile punje ya ngano (Bibi-arusi Ngano) iliyoanguka ardhini huko Nikea imerudi kwenye Neno Punje ya asili tena. Mungu na asifiwe milele. Naam, msikilizeni nabii wa Mungu aliyethibitishwa ambaye anaotokea katika wakati huu wa mwisho. Kile yeye anachosema kutoka kwa Mungu, bibi-arusi atasema. Roho na nabii na bibi-arusi watakuwa wakisema jambo lile lile. Na yale watakayosema yatakuwa tayari yamesemwa katika Neno. Wanalisema hilo sasa, "Tokeni kwake sasa mkatengwe naye." Kilio kimetolewa. Kilio kinatolewa. Sauti hiyo italia kwa muda gani? Hatujui, lakini tunajua jambo moja, haitachukua muda mrefu, kwa maana huu ni wakati wa mwisho.

Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho anayaambia makanisa. Roho amenena. Jua linalotua linakaribia kufifia katika umilele kwa ajili ya nyakati za kanisa. Ndipo lote litakuwa limekwisha. Ndipo itakuwa mtu imechelewa sana kuja. Lakini kama mahali fulani katika mfululizo wa masomo haya Mungu amekushughulikia kwa njia ya Roho Wake, naomba hata sasa umgeukie Yeye katika toba na umpe Yeye maisha yako ili kwamba kwa Roho Wake apate kukupa uzima wa milele.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7